Jumanne Juni 4, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • No. 0581697

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**MSHINDI KIMATAIFA:** Beatrice Bandawe apokewa, akitaja siri mafanikio yake

UKURASA 3



**JELA** miaka 50 kwa kubaka, magari yao yataifishwa

UKURASA 4

**DC**, diwani kikaangoni kujibu tuhuma Tume Maadili

UKURASA 5




**VINICIUS JR: NATAMANI KUBAKIA MADRID**

UKURASA 21

# Msigwa apinga ushindi wa Sugu

## ALIA na tuhuma "maelekezo ya Mbowe"; CHADEMA yamjibu; Makalla amkaribisha CCM...

Ukurasa wa 5




Mchungaji Peter Msigwa

## YALIYOMO

UKURASA WA 7

**MAJALIWA AAGIZA MAPITIO TAASISI ZA MIKOPO KUDHIBITI KAUSHA DAMU**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza wakuu wa wilaya nchini kukaa na taasisi zote zinazotoa mikopo katika maeneo husika na kuhakiki riba...

UKURASA WA 17

**SMZ YAANZA KUKABILI UHABA MADAKTARI WA WANYAMA**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeanza kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa...



**Kilichombeba Samia kutuzwa shahada ya tano udaktari**

UKURASA 2



# Mpina ataka waziri, watumishi wote wizarani wafukuzwe kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa, Luhaga Mpina (CCM), ameliomba Bunge kuitaka serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwafukuza kazi watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia waziri wake hadi mfagiaji ofisini.

Mpina alipendekeza kuchukuliwa hatua hiyo bungeni jana wakati anachangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Endelea Uk. 2

**MICHEZO** GAMONDI: MKATABA WANGU UMEMALIZIKA UK 24

MAONI, KATUNI UK.6




Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi mbalimbali wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga cha Korea pamoja wanafunzi wa chuo hicho baada ya kutunukiwa Udaktari wa Falsafa ya Heshima katika Sekta ya Anga (Honoris Causa) jijini Seoul, Jamhuri ya Korea jana. **PICHA: IKULU**

# Kilichombeba Samia kutunukiwa shahada ya tano udaktari heshima

**Na Salome Kitomari,** KOREA

CHUO Kikuu cha Sayansi ya Anga Korea (KAU), kimeeleza sababu za kumtunuku Rais Samia Suluhu Hassan Shahada ya Udaktari wa Heshima (Honoris Causa) kuwa ni kazi kubwa iliyofanyika katika kuimarisha usafiri wa anga nchini na uongozi wenye mabadiliko ya sera na kimantiki.

Kimesema R nne anazozisimamia ambazo ni Reconciliation (Maridhiano), Resiliency (Ustahamilivu), Reforms (Mabadiliko) and Rebuilding (Kujenga Upya), zimeiwezesha Tanzania kupiga hatua katika njanja mbalimbali.

Rais wa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga cha Korea, Dk. Hee Young Hurr, akizungumza jana kabla ya Samia kutunukiwa shahada hiyo, alisema ni Rais pekee mwanamke Afrika na mwanamke wa kwanza kwa nafasi hiyo Tanzania katika historia ya miaka 60 ya Tanzania ambaye alileta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii kwa kuwa na uongozi wa ushirikiano kipindi cha UVIKO- 19.

Alisema kupitia R nne, amelileta taifa pamoja na kuchangia mabadiliko na ustawi wa kijamii, huku akiwa kiongozi mashuhuri kwenye mabadiliko ya tabianchi na nishati safi ya kupikia kwa Afrika ambayo ni mafanikio makubwa kwenye sekta za afya, elimu, TEHAMA, usafiri wa anga, viwanda na miundombinu.

"Mafanikio haya ni kutokana na uongozi bora na kumfanya kujulikana kimataifa licha ya kuongoza kwa kipindi kifupi. Katika sekta ya anga kuna mabadiliko makubwa kwa vitendo hatua inayodhihirisha uongozi bora ambao umeibadili sekta ya anga kwa sasa," alisema.

Pia alisema hatua kubwa alizochukua kiongozi na uongozi wenye kujali wengine, kurekodi filamu ya The Royal Tour ambayo vimesaidia kukuza utalii duniani, kuendeleza miundombinu ya viwanja vya ndege kwa kujenga Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato, Dodoma, utakaozinduliwa Desemba, mwakani.

Eneo lingine ni uwekezaji kwenye kujenga mifumo na nguvu kazi katika kuongeza idadi ya abiria na ndege za mizigo hatua zilizosaidia nchi kuwa na ndege 14 za abiria na moja ya mizigo, hivyo kufanya ongezeko la safari za ndani na nje ya nchi kama Dubai na China.

"Kwa kutambua uongozi wake, ari ya kipekee ya Rais Samia yenye mafanikio makubwa Chuo Kikuu cha Sayansi ya Anga kimeamua kumtunukia shahada ya udaktari wa heshima," alisema.

Akizungumza baada ya kutunukiwa shahada hiyo, Rais Samia alisema amepokea kwa hisia kubwa ya uwajibikaji na kujitolea kwa Watanzania na kwamba kwa msaada wao na watangulizi wake, hasa Hayati Dk. John Magufuli ambaye aliweka misingi ya ukuaji wa sekta ya usafiri wa anga, mafanikio yanaonekana sasa.

Alisema msingi uliowekwa na Magufuli umewezesha kuendelea na kufanya mabadiliko makubwa katika kuhakikisha Tanzania inasonga mbele na kwamba amejitolea kuhakikisha sekta ya anga inabaki kuwa chachu ya maendeleo na ustawi wa nchi.

Pia alikiomba chuo hicho kushirikiana na Tanzania katika kufundisha na kubadilishana maarifa na wataalamu wa sekta ya anga Tanzania.

Rais Samia alisema kwa sasa Tanzania inaunganika na viwanja 38 duniani na kwamba kuna nafasi kubwa ya muunganisho na maeneo mengi lakini kuna changamoto mbalimbali zinazozuia kuwa wa haraka wa sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Rais Samia, sekta ya anga ya Tanzania kati mwaka 2021 hadi 2023 imekua kwa kuwa abiria wameongezeka kila mwaka kwa takriban asilimia 28 na idadi ya ndege zinazofanya safari za kimataifa zimeongezeka kutoka 26 hadi 33.

"Idadi ya wasafiri wa ndani imeongezeka kwa asilimia 26.5 baada ya UVIKO-19 kutoka abiria milioni tatu hadi milioni 3.8 kwa mwaka 2023. Nia ilikuwa kuwekeza kimkakati hasa katika kufufua Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kuendeleza miundombinu, ikiwamo mfumo wa kujenga rada, kukarabati na kupanua viwanja vya ndege nchini kote," alisema.

Alisema kabla mwaka 2016, ATCL ilikuwa na ndege moja inayofanya kazi na hadi Machi 2024, zimeongezeka ndege 14 za abiria na moja ya mizigo na kwamba ndege sita kati ya hizo, zimenunuliwa katika kipindi cha miaka mitatu ikiwamo ndege ya mizigo.

Aidha, alisema mtandao wake umepanuliwa kutoka maeneo 4 tu nchini hadi 24, ikiwamo safari katika miji minane Afrika na mitatu ya kimataifa (Guangzhou, Dubai na Mumbai).

Rais Samia alisema kufufua shirika hilo kumesaidia kuongeza mapato kutoka Sh. bilioni 23 mwaka 2016/17 hadi bilioni 380.4 mwaka 2022/23 huku soko la ATCL la safari za ndani likifika asilimia 53 kutoka asilimia 2.4 tu mwaka 2022/23. Pia idadi ya abiria imeongezeka kwa asilimia 42 kutoka milioni 4.8 mwaka 2015 hadi milioni 6.8 mwaka huu.

"Idadi ya marubani waliosajiliwa na wahandisi wa ndege imeongezeka kufikia 604 ikiwa ni ongezeko la asilimia 21 na wahandisi kufikia 76 ambao ni ongezeko la asilimia 181 mpaka mwisho wa mwaka 2023," alisema.

Rais Samia alisema mchango katika sekta ya anga kwenye pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 0.9 mwaka 2018 hadi asilimia 2.5 mwaka 2023.

Tayari kiongozi huyo ana shahada tano za udaktari wa heshima baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Zanzibar (SUZA), Chuo Kikuu cha Jawaharial Nehru cha India na Chuo Kikuu cha Ankara, Uturuki, wote wakitambua mchango wake kwenye nyanja mbalimbali.

Rais Samia amehitimisha ziara rasmi ya siku mbili na leo anaanza ziara ya kikazi na atahudhuria mkutano wa wakuu wa nchi na serikali kati ya Korea na Afrika. Katika mkutano huo, atatoa maoni katika jopo la Kuimarisha Usalama wa Chakula na Madini.

# Mpina ataka waziri, watumishi wote wizarani wafukuzwe kazi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MBUNGE wa Kisesa, Luhaga Mpina (CCM), ameliomba Bunge kuitaka serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kuwafukuza kazi watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia waziri wake hadi mfagiaji ofisini.

Mpina alipendekeza kuchukuliwa hatua hiyo bungeni jana wakati anachangia mjadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema moja ya maeneo ambayo yamekuwa na kero katika wizara hiyo ni wananchi wanaoishi pembezoni mwa hifadhi kubambikwa kesi, kuteswa, mifugo yao kukamatwa na wengine kuuawa.

"Kumekuwapo tabia ya wananchi wanaoishi maeneo ya pembezoni mwa hifadhi kubambikwa kesi, wengine kukamatiwa mifugo yao, kunyanyaswa na wengine hata kuuawa na watumishi katika hifadhi zetu.

"Mimi nilishaleta ushahidi hapa bungeni na Waziri Mkuu akatoa maagizo 12, hakuna kilichofanyiwa kazi, manyanyaso yanaendelea kwa wananchi wetu wanaoishi katika maeneo ya pembezoni mwa hifadhi," alisema.

Mpina alisema hata katika taarifa ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii iliyowasilisha bungeni Ijumaa iliyopita, inaeleza juu ya ukubwa wa tatizo hilo la wananchi kubambikwa kesi.

"Tena Kamati ya Bunge yenyewe imenukuu hadi mahakama kuonesha kuchoshwa na vitendo vya wananchi wanaoishi maeneo jirani na hifadhi kuwabambika kesi.

"Sasa kama maelekezo ya Waziri Mkuu yamepuuzwa na malalamikio yetu wabunge, basi wabunge wenzangu niwaombe leo (jana) tutoe fundisho. Niwaombe leo tuitake serikali kupitia kwa Waziri Mkuu kufukuza watumishi wote wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzia waziri hadi mfagiaji wa ofisi ili iwe fundisho," alisisitiza Mpina.

Vilevile, mbunge huyo alishauri Bunge kuunda kamati itakayofanya uchunguzi katika hifadhi zote zilizo pembezoni na vijiji vya watu ili kukomesha matukio hayo.

Mpina alihoji kuhusu wizara hiyo kukaa kimya juu ya tukio la mamba ambaye aliuawa na mwindaji kutoka Marekani anayedaiwa kuwa ndiye alikuwa mrefu kuliko wote duniani.

"Tumekuwa tukitafuta vivutio vya watalii lakini kama kweli tulikuwa na mamba mwenye urefu kuliko wote duniani kwanini tuliruhusu auawe? Kwanini tusingemjengea kizimba na kujenga kituo cha utalii pale?

"Lakini tangu kutokea kwa tukio hili hakuna mamlaka ambayo imewahi kujitokeza kukanusha kuwa mamba huyo hakuwa ndiye mrefu kuliko wote duniani. Hii inaonesha kuwa kuna njama ambazo watumishi ndani ya wizara wamefanya kulihujumu taifa kwani inaonesha wazi walikuwa wanajua huyo ndiye mamba mrefu kuliko wote," alisema.

Alitaka hatua zichukuliwe dhidi ya wote waliohusika na uchunguzi ufanyike ili kubaini nini kilitokea hadi mamba mwenye urefu wa sentimita 493.8 kuuawa kwa kibali cha mamba wa kawaida.

"Waziri na TAWA (Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori, kwanini walikubali mamba mwenye urefu huu wa sentimita 493.8, karibu mita tano auawe na mwindaji ambaye alionekana kwenye vyombo vya habari akijiita kuwa amewinda mamba mrefu kuliko wote duniani na baadaye kumchuna ngozi?

"Je, huyu mamba alikuwa na thamani kama mamba wengine, nchi yetu haikuwa na matumizi na mamba huyo?" Mbunge Mpina alihoji.

Mbunge wa Njombe, Deo Mwanyika (CCM) alitaka serikali kuangalia upya vibali vya uvunaji misitu ambavyo wamekuwa wanatoa kwa wawekezaji.

Alisema hivi sasa kuna uvunaji ambao hauzingatii utunzaji mazingira, wananchi hawanufaiki na misitu yao kwa kuwa wawekezaji hao wamekuwa wao ndiyo wapanga bei.

MSHINDI WA KIMATAIFA:

# Beatrice Bandawe apokewa, akitaja siri ya mafanikio yake

**Na Jenifer Gilla**




Mratibu wa Mradi wa Mafunzo ya Uongozi kwa Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, Dk. Joyce Bazira (kushoto), akimpa maua ya pongezi Mhariri Mtendaji wa Gazeti Nipashe, Beatrice Bandawe, iliyoandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA) jijini Dar es Salaam jana. Bandawe alitunukiwa tuzo na Shirika la Kimataifa la WAN-IFRA/Women in News hivi karibuni. **PICHA: JENIFER GILLA**

MSHINDI wa Tuzo ya Kimataifa ya Uongozi Katika Vyombo vya Habari, Beatrice Bandawe, ametoa siri ya matumizi sahihi ya jinsia kitaaluma; mwandishi apangiwe majukumu kulingana na uwezo wake na si jinsia.

Beatrice, Mhariri Mtendaji wa Gazeti Nipashe, amesema dhana ya kupanga majukumu kwa kuzingatia jinsia inadumaza taaluma za wafanyakazi, hasa wale ambao hawapangiwi majukumu.

Mshindi huyo alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kumpongeza kwa kupata tuzo hiyo ya kimataifa, aliyokabidhiwa tarehe 29 mwezi uliopita jijini Copenhagen, Denmark na Jumuia ya Wachapishaji Duniani (Wan-Infra).

"Kuna wakati mwanamke anaweza kuleta habari za maudhui fulani, lakini kwa vile ofisi inaona kuwa mwanamke hana uwezo wa kuleta maudhui hayo, ananyimwa nafasi ya kuonesha uwezo wake," alifafanua Beatrice.

Vilevile, katika mustakabali huo wa jinsia, Mhariri Mtendaji Beatrice alisisitiza mfumo wa uandishi wenye maudhui yanayoegemea uwiano sawa wa sauti za wanawake na wanaume, ili makundi hayo yapate nafasi sawa za kufikishwa ujumbe wao kijamii, zikitafutiwa suluhisho.

Alitoa ushauri wa kitaalamu kwamba, umefika wakati juhudi za kipekee zifanywe kwa kupaza sauti za makundi anayoyataja "sauti zao hazisikiki", wakiwamo wenye ulemavu, ili wapate mwamko wa kuwa washiriki hai katika vyombo vya habari.

Mratibu wa Mradi wa Mafunzo ya Uongozi kwa Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, unaotekelezwa na Shirika la Kimataifa la WAN-IFRA/ Women in News, Dk. Joyce Bazira alisema ushindi wa Beatrice, ni wa kujivunia kitaifa.

Alifafanua kwamba ni mara ya kwanza tuzo hiyo kutolewa kwa mwanahabari nchini na mara ya nane kwa mabara ya Afrika na Asia.

Kwa mujibu wa Dk. Joyce, nchi za Afrika zilizokwishapata tuzo hiyo anayoitaja ni yenye ushindani mkubwa ni: Kenya, Uganda, Zambia, Zimbabwe, Botswana, Nigeria na Sudan Kusini.

Binafsi, Dk. Joyce aliyekwishatumika na Beatrice katika chombo kimoja cha habari, alimsifu kwamba tuzo aliyotunukiwa inabeba ishara ya utendaji bora na utayari kikazi, sambamba na kufanyia kazi mafunzo ya uongozi aliyopata na anayoendelea kuyapata.

"Kama kocha niliyempatia Beatrice mafunzo ya uongozi, ninajivunia kuona anapata tuzo inayoashiria kiongozi aliyeleta mabadiliko chanya kwenye chombo cha habari. Hii inaonesha kuwa yale tunayomwelekeza anayafanyia kazi," alisema Dk. Joyce.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben alimpongeza Beatrice kwa kuiletea nchini tuzo hiyo, ambayo sifa yake imetetea bara zima la Afrika.

Akatumia fursa hiyo kuelekeza motisha ya sifa ya Beatrice, kwa wanahabari wanawake nchini kufanya kazi na kujikweza kitaaluma hadi kufikia wasifu wa michango yao kubeba sifa za kimataifa.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com



**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5

For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Jela miaka 50 kwa kubaka, utakatishaji fedha

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Lindi imewahukumu kutumikia kifungo cha miaka 30 gerezani kwa kosa la ubakaji na miaka 20 kwa kosa la utakatishaji fedha pamoja na kulipa fedha Sh. milioni 35 walizoiba, huku mali zao zikitaifishwa.

Waliohukumiwa ni Kazil Hamis (43), mkazi wa Dar es Salaam na John Mkondo 'Kikwete' (51), mkazi wa Morogoro.

Hukumu hiyo ilitolewa Mei 31, 2024 na Hakimu Mkazi Mfawidhi Consolata Singano wakati kesi hiyo ilipokuja kwa ajili ya kutolewa hukumu.

Awali jopo la mawakili wa serikali likiongozwa na Wakili Godfrey Mramba lilidai kuwa walikuwa na mashahidi 32 na vielelezo 35 vilivyowatia hatiani washtakiwa wote.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, washtakiwa kwa pamoja walikabiliwa na mashtaka 16.

Wakili Mramba alidai kuwa katika shtaka la kwanza la kula njama ya kutenda kosa la wizi washtakiwa wote hawakukutwa na hatia.

Katika shtaka la pili na la tatu la kubaka, ilidaiwa kuwa mnamo Machi Mosi, 2022 katika Hoteli ya White Pearl iliyoko Mtaa wa Mikumbi, wilaya na mkoa wa Lindi, pasipo na ridhaa washtakiwa waliwabaka waathirika wa kwanza na wa pili (majina yamehifadhiwa) wakiwa katika hali ya kutokujitambua.

Kosa la nne, tano, sita ni wizi. Ilidaiwa kuwa mnamo Machi Mosi, 2022 katika Hoteli ya White Pearl, wawili hao waliiba pete ya dhahabu yenye uzito wa gramu 12, yenye thamani ya Sh. milioni 1.8, simu moja ya mkononi aina ya Samsung S7 Edge yenye thamani ya Sh. milioni 1.5, kadi ya benki ya CRDB yenye namba 0152.... kadi ya benki ya NMB yenye namba za akaunti 20..... na fedha Sh. 300,000, vitu vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 3,6, mali ya mwathirika wa kwanza (jina limehifadhiwa).

Pia Machi Mosi, 2022 katika Hoteli ya White Pearl, walidaiwa kuiba saa moja aina Oriflame, yenye thamani ya Sh. 180,000, simu moja ya mkononi aina ya Infinix Hot 11 yenye thamani ya Sh. 510,000, fedha taslimu Sh. 120,000, vitu vyote vikiwa na thamani ya Sh. 810,000, mali ya mwathirika wa pili (jina limehifadhiwa).

Pia iilidaiwa mahakamani huko kuwa kati ya Machi Mosi, 2022 na Machi 2, 2022 katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Lindi na Mtwara, waliiba fedha taslimu Sh. milioni 35 kwenye akaunti ya benki ya CRDB yenye namba 0152.... na akaunti ya benki ya NMB yenye namba za 2010240.... mali ya mwathirika wa kwanza (jina limehifadhiwa).

Kati ya tarehe zilezile na maeneo yaleyale, washtakiwa kwa pamoja waliiba fedha taslimu Sh. 120,000 kwenye laini ya simu ya Tigo, mali ya mwathirika wa pili.

Ilidaiwa kuwa mnamo Machi 2 2022, eneo Masasi katika Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, kwa makusudi na wakiwa na nia ya kuhadaa waliwasilisha nyaraka ya uongo ikiwa ni fomu ya kutolea fedha ya benki ya NMB yenye jina la mwathirika wa kwanza ikiwa imejazwa kiasi cha Sh. milioni tatu kwa Wakala wa NMB wakiaminisha kuwa ni nyaraka ya kweli ya kutolea kiasi cha fedha kilizojazwa huku wakijua kitendo hicho ni kosa kisheria.

Pia iliendelea kudai kuwa eneo na tarehe hiyo hiyo washtakiwa kwa makusudi na wakiwa na nia ya kuhadaa waliwasilisha nyaraka ya uongo ikiwa ni fomu ya kutolea fedha ya benki ya NMB yenye jina la mwathirika wa kwanza ikiwa imejazwa kiasi cha Sh. 4,000,000 kwa Nassoro Saidi Selemani, wakala wa NMB, akiaminisha kuwa ni nyaraka ya kweli ya kutolea kiasi cha fedha kilichojazwa.

Kosa la 12, 13 na 14 ni kutumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la mtu mwingine. Ilidaiwa kuwa Kazili Hamis, mnamo Juni 30, 2022, eneo Tegeta, wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, alitumia laini ya simu iliyosajiliwa kwa jina la Sharifa Jonas Hyera pasipokumjulisha mtoa huduma.

Katika kosa la 15 ni la kutakatisha fedha. Ilidaiwa kuwa kabla au baada ya Juni 30, 2022 eneo lisilofahamika katika Mkoa wa Dar es Salaam, kwa nia ya kuficha chanzo halisi Hamis alitakatisha Sh. milioni 35 kwa kununulia gari aina ya Toyota Aphard Na. 548 DZQ huku akifahamu fedha hizo ni mazalia ya uhalifu wa wizi.

Kosa la 16 ni kutakatisha fedha, ilidaiwa kuwa washtakiwa wote kwa pamoja tarehe tofauti kati ya Machi Mosi, 2022 na Machi 2, 2022, maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Lindi na Mtwara, walijipatia fedha Sh. milioni 35 huku wakifahamu fedha hizo ni mazalia ya uhalifu wa wizi.

Mahakama iliamuru mshtakiwa wa kwanza na wa pili kuwalipa waathirika wa kwanza na wa pili fidia ya Sh. millioni tano kwa kila mmoja. Pia kurudisha kiasi cha Sh. milioni 35 kwa waathirika.

Vilevile, magari matatu yametaifishwa na kuwa mali ya serikali ambayo ni Toyota Alphard lenye namba za usajili T. 548 DZQ, Nissan Dualis lenye namba za usajili T. 141 DWA na Toyota IST lenye T. 978 DJD.

Mahakama pia imeamuru gari moja aina ya Toyota IST lenye namba za usajili T 531 DVA lirudishwe kwa mwenyewe (mmiliki) ambaye hakuwa mshtakiwa katika shauri hilo.

**Pia Machi Mosi, 2022 katika Hoteli ya White Pearl, walidaiwa kuiba saa moja aina Oriflame, yenye thamani ya Sh. 180,000, simu moja ya mkononi aina ya Infinix Hot 11 yenye thamani ya Sh. 510,000, fedha taslimu Sh. 120,000, vitu vyote vikiwa na thamani ya Sh. 810,000, mali ya mwathirika wa pili (jina limehifadhiwa).**



# DC, Diwani kikaangoni madai ukiukwaji maadili

**Na Joseph Mwendapole**

SEKRETARIETI ya Maadili ya Viongozi wa Umma, imepanga kuwafikisha mbele ya baraza hilo, Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi, Onesmo Buswelu na Diwani wa Cheyo, Manispaa ya Tabora, Yusuph Kitumbo, kwa tuhuma za ukiukaji wa maadili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamishna wa Sekretarieti hiyo, Jaji Mstaafu Sivangilwa Mwangesi, viongozi hao watafikishwa mbele ya baraza hilo Juni 7 kwa tuhuma za ukiukaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Taarifa hiyo ilisema kikao hicho cha kusikiliza tuhuma dhidi ya viongozi hao, kitafanyika kwenye ukumbi wa mikutano ulioko kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, kuanzia asubuhi.

Shauri hilo, kwa mujibu wa taarifa hiyo, litasikilizwa kwa uwazi na wananchi wote wanaotaka kusikiliza wataruhusiwa bila pingamizi lolote.

"Baraza la maadili linatarajia kufanya kikao cha uchunguzi wa kina wa malalamiko kwa mujibu wa kanuni ya 11 ya kanuni za maadili ya viongozi wa umma kwa viongozi hawa ili haki iweze kutendeka," ilisema.

Moja ya majukumu ya sekretarieti hiyo ni kuchunguza tabia na mienendo ya kiongozi yeyote kwa lengo la kuhakikisha masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa.

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ni taasisi inayojitegemea chini ya Ofisi ya Rais iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 132 ya Katiba ya mwaka 1977.

Hivi karibuni, sekretarieti hiyo ilisema baadhi ya viongozi kutoa ufafanuzi wa vyanzo vya mapato waliyo nayo na wameshindwa kutaja thamani ya mali walizo nazo kwenye fomu ya tamko la mali.

Ilisema baadhi ya viongozi wameshindwa kujaza taarifa za wenza wao hasa taarifa za fedha zilizoko benki na wameshindwa kujaza vipengele muhimu huku wengine wakipokea zawadi mbalimbali bila kuzitolea matamko.

Dosari hizo, ilisema zinatoa taswira kwamba baadhi ya viongozi bado hawana uelewa wa kutosha kuhusu namna ya kujaza matamko ya mali na masuala yanayotakiwa kuainishwa.




Mkurugenzi Mtendaji wa EATV Ltd, Regina Mengi, akitia saini makubaliano na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Dk. Erasmus Kipesa, katika uzinduzi wa kampeni ya Namthamini inayoendeshwa kwa pamoja kati ya EATV na TEA kuhamsisha jamii kuchangia ununuzi wa taulo za kike, ujenzi wa vyoo na huduma za maji ili kuwezesha wanafunzi wa kike kusoma katika mazingira rafiki. Utiaji saini huo ulifanyika katika ofisi za studio za EATV, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Unaweza kuchangia kupitia Airtel Money 0787-633313 jina East Africa Television au kwa Lipa Namba (M-Pesa) 5999900 jina East Africa Television. Pia unaweza kuleta mchango wako katika ofisi za East Africa Television zilizoko Mikocheni, Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msigwa apinga ushindi wa Sugu

**Na Francis Godwin,** IRINGA

AKIYEKUWA Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa, Mchungaji Peter Msigwa, amekata rufani kupinga matokeo ya uchaguzi uliompa ushindi Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu.

Msigwa amedai huwa katika uchaguzi huo uliofanyika Makambako mkoani Njombe wiki iliyopita, kulikuwa na ukiukwaji wa kanuni za katiba katika upigaji kura pamoja na kufanyika kwa fujo ambazo zilichangia kuharibu uchaguzi huo.

Katika uchaguzi huo, alisema kulikuwa na mambo mengi ambayo ni kinyume cha kanuni za uchaguzi za chama hicho, ikiwamo wapigakura kuitwa nje kushawishiwa kumchagua mpinzani wake kwa kile kilichodaiwa ni maelekezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Taifa wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Akizungumza jana na waandishi wa habari nyumbani kwake, Kihesa Kilolo, mjini hapa, Msigwa alisema kama chama kitashindwa kufanyia kazi barua yake ya kukata rufani, kitashindwa kujitofautisha na Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika uminyaji wa demokrasia na haki.

Msigwa pia alikishauri chama hicho kijitafakari upya na kurudi katika misingi yake ya haki na demokrasia kwa kuheshimu mawazo ya watu wote wakiwamo wanachama bila kuwapinga na kuwapuuza kwa kuwa kupishana kwa hoja ndio ukomavu wa kisiasa.

Hata hivyo, mwanasiasa huyo ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Iringa Mjini kwa vipindi viwili, alikanusha madai ya kuhama chama. Alisema kamwe hawezi kuhama na kusisitiza kwamba ataendelea kupambana ndani ya chama huku akiwaambia wale wote waliokuwa wanatarajia atatangaza uamuzi huo wataondoka na kumwacha.

"Katiba ya CHADEMA inafafanua vizuri wanaopaswa kupiga kura ni wenyeviti makatibu wa mabaraza ya chama ambayo ni wanawake, vijana na wazee.

"Waliosimamia uchaguzi huu waliwazuia makatibu kupiga kura jambo ambalo ni kinyume cha katiba. Kwa hiyo nimekata rufani kwenye chama changu kwamba hao ambao walipaswa kupiga kura yaani makatibu watatu wa mabaraza walizuiwa kupiga kura. Ukiangalia kura zilizoongezeka za kwangu zilikuwa sita, watatu hawakuruhusiwa kupiga kura," alisema.

"Kama CHADEMA tunalalamikia CCM, tunalalamikia serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwamba wasimamizi wa uchaguzi huwa hawatendi haki, CHADEMA tulitakiwa tuwe mfano wa kuigwa kwamba katika uchaguzi wanaosimamia wanatenda haki. Sasa kama mimi mjumbe wa kamati kuu ninatoa malalamiko haya halafu hayasikilizwi tena ndani ya chama chenye kutenda haki, nani atasikilizwa?" alisisitiza.

Msigwa pia alimlalamikia Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA (Bara), Benson Kigaila, aliyekuwa msimamizi wa uchaguzi huo kwa kutokuchukua hatua yoyote dhidi ya watu waliofanya fujo wakati wa mchakato huo.

"Hali ile inaleta shida na mashaka na harufu ya uvundo wa ukiukwaji mkubwa wa haki ndani ya chama chetu," alisema Msigwa.

Hata hivyo, mmoja wa wanachama wa CHADEMA Iringa, Kabambe Temihanga, alimtaka Mchungaji Msigwa kutulia na kumwacha Sugu kufanya kazi ya kujenga chama kwa kuwa demokrasia imechukua mkondo wake na kuhoji iwapo angeshinda yeye ingekuwaje?

Pia alisema rafu za uchaguzi huo zilianza toka uchaguzi wa ngazi za chini na yeye akiwa mwenyekiti wa kanda ila maumivu ambayo wanachama wa chini wamepata ndio ambayo yamemrudia.

**CHADEMA YAJIBU**

Akizungumzia tuhuma hizo za Mch. Msigwa, Mkurugenzi wa Uenezi na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema, "tuhuma zinapaswa kuwa na ushahidi na si maneno maneno!" (Mch. Msigwa) anapaswa kuwasilisha ushahidi wake katika rufani yake ambayo anasema ameikata.

"Kauli ya chama ni kwamba, kwa sasa tunasubiri hiyo rufani yake ili iweze kufikishwa kwenye mamlaka husika, ila suala la rufani si jipya katika chama chetu, ni utaratibu wa kawaida ndani ya chama."

Mremba aliwataka wanachama waendelee na majukumu ya kujenga chama, hasa kipindi hiki ambacho wanajipanga kwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**CCM YAMWITA**

Kukiwa na hali hiyo CHADEMA, CCM imemkaribisha Mch. Msigwa kujiunga nacho kama hakubaliani na yanayoendelea ndani ya chama hicho cha upinzani.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Soko la Kilombero, jijini Arusha, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, alimtaka Msigwa kwenda CCM ambako alidai kuna demokrasia.

Mkutano huo ni mwendelezo wa ziara ya Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye anatembelea mikoa mitano kusikiliza kero za wananchi na kuzitolea ufumbuzi wake.

Katika mkutano huo, Makalla alimnukuu Mch. Msigwa akisema, "Ninajitokeza hadharani kuwaeleza Watanzania na wana CHADEMA sisi muda wote tumehoji Tume ya Uchaguzi kumbe sisi ni waongo, hata sisi wenyewe hatufuati taratibu za uchaguzi, mimi nimeonewa, nimeibiwa kura".

Makalla akimjibu Msigwa, akisema "Na mimi ninamwambia Msigwa 'pole sana mchungaji, njoo CCM ambako kuna demokrasia tele, kuna uwazi. Umeonewa, pole sana Mch. Msigwa, hicho chama hakikufai tena, njoo CCM'".

Makalla alisema Msigwa amesema huwa wanawadanganya watu kuhusu katiba, tume ya uchaguzi, kumbe CHADEMA haifuati sheria za uchaguzi.

"Kwa hiyo mnaweza kuona wenzetu sasa wana mgogoro mkubwa, hakukaliki mnawasikia wanaleta ubaguzi, ni stress (msongo wa mawazo), kuna mgawanyiko mkubwa ndani ya CHADEMA.

"Na sisi CCM tunaamini kwamba adui yako mwombee njaa, kwa jirani kunawaka moto, hakuna haja ya kupeleka maji. Sisi tungependa kuwa na vyama vya upinzani vyenye nguvu, lakini katika hili tunaiona fursa ya CCM kushinda Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kushinda Uchaguzi Mkuu unaokuja," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto visifumbiwe macho

**KILA** uchao kumekuwa na taarifa kuhusu ukatili dhidi ya watoto ambao unafanywa na watu wa karibu wa familia wakiwamo ndugu wa mama au baba ambao wanaishi nao. Vingine vinafanywa na watu ambao wameaminiwa kama vile walimu wanaowafundisha shuleni au kwenye masomo ya dini.

Vitendo hivyo kama vile watoto kunajisiwa, kulawitiwa na kubakwa kwa sasa vinaripotiwa maeneo mbalimbali ya nchi jambo ambalo linaonyesha kuwa ni tatizo kubwa katika jamii. Licha ya kuwapo kwa sheria kali ambayo mtu akibainika kujihusisha na vitendo hivyo, adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela, bado kasi ya kuongezeka kwa matukio hayo ni kubwa.

Kuendelea kuota mizizi kwa vitendo hivyo ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za wanafamilia kulindana kwa hofu kwamba iwapo mhusika atatangazwa familia husika inaweza kutengwa kwenye ukoo, kesi kumalizwa kimyakimya na polisi au ofisi za serikali za mitaa na rushwa kwa familia ya mhusika kuipoza familia au mtoto aliyeathirika kwa kupewa fedha.

Aidha, katika mkutano wa wanaharakati na wadau wa kupinga ukatili Zanzibar mapema mwaka huu, ilielezwa kuwa moja ya sababu ni mashahidi kutokufika mahakamani pindi kesi inapofikishwa kwenye sheria kwa kuhofia lawama au athari kama vile kupigwa au kuuawa na watuhumiwa baada ya kutoa ushahidi.

Katika mitandao ya kijamii, kuna taarifa ambayo inasambaa ikimwonyesha Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Aziza Mangosongo, akieleza kukithiri kwa vitendo hivyo ndani ya kisiwa hicho. Katika taarifa hiyo aliyoitoa wakati wa ziara ya Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Zaynab Vullu, mkuu huyo wa wilaya amesema kuna watoto 15 waliolawitiwa na mwalimu wa madrasa.

Mangosongo hakuishia hapo tu bali alisema mtoto mmoja amelawitiwa na baba wa kambo huku watoto wengine sita wakifanyiwa vitendo kama hivyo kwa nyakati tofauti. Sambamba na vitendo hivyo, kiongozi huyo alibainisha kuwa wanafunzi kadhaa wa kike wamepatiwa ujauzito na walipokaguliwa zaidi wameonekana wameingiliwa kinyume cha maumbile. Wakati akiweka hayo bayana, mkuu huyo wa wilaya alisema vitendo kama hivyo ndani ya kisiwa hicho ni vingi na vinazidi kushamiri kila siku na baadhi ya wahusika wanafahamika lakini wanalindwa na jamii inayowazunguka.

Kwa ujumla vitendo hivyo vinalitia doa taifa lakini pia vinasababisha madhara makubwa katika jamii. Kasi hiyo inaashiria kuwa jitihada zaidi zinatakiwa ili kuhakikisha zinatokomezwa ndani ya jamii.


Katika kufikia malengo ya kutokomeza ukatili huo, familia ndiyo msingi kwa wazazi kutenga muda na kuzungumza na watoto wao kuhusu kujilinda na kujiepusha. Kwa sasa ndani ya familia nyingi, wazazi wameacha kukaa na watoto badala yake jukumu hilo wamewaachia wafanyakazi wa ndani na walimu na walezi shuleni ambao pia baadhi yao si waaminifu.

Msemo kwamba familia ni msingi wa maendeleo, amani na ustawi katika jamii, hivi sasa umepewa kisogo kwa kuwa wazazi muda mwingi wanautumia kwa kutafuta fedha na hata wawapo nyumbani ni nadra kuzungumza kwa sababu wanakuwa zaidi kwenye mitandao ya kijamii kwa kutumia simu za kiganjani. Ni vyema sasa familia ikarejea katika mstari wake ili kuelekeza nguvu katika malezi ya familia.

Aidha, mke wa Rais Mstaafu, Mama Salma Kikwete, aliwahi kuibuka na msemo kwamba mtoto wa mwenzio ni wako. Kwa kauli hiyo, jamii inahusika moja kwa moja katika kuwalinda watoto dhidi ya hatari za kubakwa, kunajisiwa au kulawitiwa na watu wanaojihusisha na vitendo hivyo.

Jamii pia inapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuwafichua watu wanaowaharibu watoto kwa kuwafanyia vitendo hivyo vya kinyama na kuwafikisha katika vyombo vya sheria. Kwa jumla, vitendo hivi katu havipaswi kufumbiwa macho na jamii. Kila mtu anapaswa kuwa mlinzi wa watoto dhidi ya majanga haya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Jane Mathias

# Mbona hatujishirikishi tunabaki kulalamika

**KUMEKUWA** na malalamiko kutoka kwa wazazi na walezi kuhusu uhaba wa miundombinu mfano madawati katika shule za umma za msingi na sekondari, unaolazimisha wanafunzi wengi kukaa chini.

Malalamiko hayo na mengine sugu yamekuwa yakitolewa dhidi ya serikali, huku wengi wao wakiishutumu kushindwa kuyatatua kwa madai ya ukosefu wa fedha.

Upungufu huo ni sehemu ya vyanzo vya kushusha na kuzidi kuporomoka kiwango cha elimu kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya kitaifa.

Yote hayo yakitokana na mazingira ya kujifunza na kufundisha kuwa duni.

Aidha, kuna wazazi na walezi ambao pia wamekuwa wakipinga kuchangia chakula kwa wanafunzi shuleni wakidai kazi hiyo inapaswa kufanywa na serikali.

Ili kukabiliana na hilo la wanafunzi kupata chakula cha mchana kumezilazimu shule nyingi kupitika vikao vya kamati zinazoundwa na wazazi na walezi wa wanafunzi kukubaliana kuchangia kiasi cha fedha au chakula kwa kila mwanafunzi ili apate mlo wa mchana na kuendelea na masomo.

Hata hivyo wapo ambao wanalalamika kuwa kiasi wanachotoa kila siku kwa kila mwanafunzi kugharamia chakula cha mchana hakilingani na chakula watoto wao wanachopata.

Wanalalamika kuwa kiasi hicho wanachoingia kwa siku kinapaswa kuwapa mlo unaolingana na fedha waliyotoa wakitoa mfano wa kulishwa makande na ubwabwa kwa maharage.

Kuna shule ambazo zimeweka utaratibu wa kuzuia mwanafunzi kuingia kwenye eneo la shule kwa kuweka mlinzi getini anapokosa fedha iliyopangwa na kamati hizo.

Ikumbukwe akizuiliwa hukosa masomo, hali ambayo inachangia pia kukithiri kwa utoro kwa wanafunzi kwa kisingizio hicho.

Ikumbukwe serikali inatatua changamoto nyingi kwa shule zake ikiwa ni pamoja na uhaba wa madarasa, shule kulingana na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu ya msingi, sekondari na hata ya kidato cha tano na sita ambao wamekuwa wakiongezeka kila mwaka.

Vilevile, imekuwa na jukumu la kuhakikisha inaajiri walimu wa kutosha kuwapa elimu bora wanafunzi ili kupata wataalamu wa leo na kesho wakiwamo madaktari, wanahabari, walimu na wahandisi.

Tunapaswa kufahamu ya kwamba, serikali ili kufanikisha mipango hiyo na mingine katika sekta zake nyingine imekuwa ikitumia fedha nyingi.

Mfano imekuwa ikijenga miundombinu mbalimbali ikiwamo ya maji, barabara, umeme, simu na viwanja vya ndege kwa kutumia fedha ambazo imekuwa ikikusanya kodi kutoka kwa wananchi.

Pia zipo za misaada ya wafadhili na mikopo kutoka kwa benki na taasisi za fedha ambazo baadaye inatakiwa kuzirejesha kwa makubaliano ya vipindi maalumu.

Sisi wazazi na walezi tunapaswa kuelewa kwamba ni jukumu letu kusaidiana na serikali kwa kutatua baadhi ya changamoto ikiwamo kukabiliana na uhaba wa madawati kwa kukubali kuchangia kiasi cha fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo.

Tukae katika kamati zetu za shule kwa ajili ya kupanga jinsi ya kushirikiana kutatua changamoto hizo na nyingine kwa ajili ya ustawi wa elimu bora kwa watoto wetu huku serikali nayo ikipambana kukabiliana na changamoto nzito zinazohitaji mabilioni ya serikali.

Kwani mzazi na mlezi anapokwepa kushiriki kutatua changamoto zinazozikabili shule wanazosoma watoto wao ni sawa na kumfanyia mwanawe vitendo vya ukatili na unyanyasaji kwa mfano kukaa chini kwa kukosa madawati na chakula cha mchana.

Lah sivyo kama mzazi au mlezi anaona kulipia chakula gharama basi aombe kibali cha kumpelekea mtoto wake chakula shuleni wakati wa mchana ili aweze kupata uelewa anapokuwa anafundishwa darasani.

Ikumbukwe kwamba kumkalisha mwanafunzi chini kunampunguzia uelewa anapofundishwa kutokana na mazingira anayokumbana nayo kuwa magumu.

Ingawa Waswahili wanasema shibe na mwana malevya endapo mwanafunzi atakula hadi kuvimbiwa kama ambavyo baadhi ya wazazi wanavyo taka, vivyo hivyo japo njaa ni mwana malegeza, madhara yake huchangia mwanafunzi kukosa usikivu darasani, hivyo kidogo atakachopata tumboni, kitahamsha ufahamu wake kichwani.

# Washikiliwa polisi tuhuma za kuvunja maduka, kuiba mali

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu sita akiwamo mlinzi aliyekuwa kwenye lindo na wengine wawili wanasakwa kwa tuhuma za kuvunja maduka zaidi ya 25 kwa kupanda juu ya mapaa kung'oa mabati na kuiba mali zilizokuwamo ndani ya maduka hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kwenye eneo la Kikosi cha Kuzuia Fujo (FFU), Mahenge Manispaa ya Songea, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Marko Chilya, alisema katika hali isiyo ya kawaida mjini humo kumejitokeza vitendo vya kuvunja maduka ya wafanya biashara kwa kupitia kwenye mapaa ya bati kwa kung'olewa na kuiba mali za wafanyabiashara.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kufanya operesheni kwa kuwasaka wote wanaojihusisha na uhalifu huo na tayari baadhi yao wamekamatwa na wengine wawili wanaendelea kusakwa.

Kamanda Chilya alisema kupitia operesheni hiyo wamewakamata baadhi ya watuhumiwa ambao majina yao yamehifadhiwa kwa upelelezi, wanaodaiwa kujihusisha na vitendo vya wizi na uvunjaji maduka katika maeneo ya Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Alisema wamekamata simu tatu zilizokuwa zimeibiwa katika maduka yaliyovunjwa, mabunda ya sigara, kompyuta 12 desk top, pamoja na pikipiki 10 zinazodhaniwa kuwa ni za wizi na operesheni hiyo ni endelevu.

Kamanda Chilya ametoa wito kwa wafanyabiashara wenye maduka kuacha tabia ya kuwaajiri walinzi bila kujihakikishia tabia zao na waepuke kuwaajiri walinzi wenye umri mkubwa.

Pia, aliagiza maduka yote nyakati za usiku ziwekwe taa mbele na nyuma na kamera za kificho ili ziweze kusaidia tatizo linapojitokeza na amewaomba raia wema waendelee kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu ili Mkoa wa Ruvuma uendelee kuwa salama wakati wote.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanyabiashara mkoani Ruvuma (JWT), Isaya Mbilinyi, aliiambia Nipashe kwa njia ya simu kuwa hali ni mbaya na baada ya kuona tatizo hilo linaendelea kutokea alilazimika kuitisha mkutano wa wafanyabiashara mjini Songea na kumualika Mkuu wa Polisi Wilaya Songea.



Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo, akitembelea daraja lililobomoka na mvua Kiwira wilayani Ileje jana ili kuhakikisha wakala wa barabara mijini na vijijini wanaendelea na matengenezo. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

# Majaliwa aagiza mapitio taasisi za mikopo kudhibiti kausha damu

**Na Vitus Audax**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa ameagiza wakuu wa wilaya nchini kukaa na taasisi zote zinazotoa mikopo katika maeneo husika na kuhakiki riba zinazotozwa na taasisi hizo ili kubaini na kudhibiti mikopo ya 'kausha damu'.

Aliagiza hayo juzi mkoani Geita baada ya kuweka jiwe la msingi katika jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Nyangwale ambalo ujenzi wake umefikia asilimia 85 ukigharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.7.

Majaliwa alisema serikali imekuwa inapokea malalamiko mara kwa mara kutoka kwa wananchi juu ya riba zinazotozwa na taasisi husika.

"Wananchi wanaumia kwenye riba, wamefika mahali wameanza kuita majina ya mikopo kausha damu. Mkuu wa Wilaya wakati wowote kutana na taasisi hizi uliza riba, jihakikishie kama kweli haziumizi wananchi," aliagiza Majaliwa.

Alielekeza jengo jipya la kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi lililojengwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lililopo chini ya ofisi yake litumiwe kutoa elimu ya biashara na ujasiriamali kwa wananchi pamoja na kutoa mikopo ili kujiendeleza kiuchumi.

"Pia undeni vikundi ili mnufaike na mikopo inayotolewa na serikali, vikundi vinakopesheka kwa urahisi, hata anuani yake ni rahisi pia," alisema Majaliwa.



Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu Majaliwa ameagiza watendaji wa serikali kuacha tabia ya kukaa ofisini, bali waende katika maeneo ya wananchi kutatua matatizo ya wananchi badala ya kusubiri viongozi wa juu kupokewa na mabango.

"Siku zote za wiki ni vijijini, kukutana na wananchi kusimamia miradi, kusikiliza na kutatua matatizo yao. Wananchi hawa hawapaswi kusubiri Waziri Mkuu, Makamu wa Rais au Rais ndio waje na mabango ukilisoma anasema nimenyang'anywa kiwanja changu wakati wa kuvishughulikia yupo hapa," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu pia alimwagiza Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Geita ahakikishe analitokomeza kundi la kihalifu maarufu mazombi ambalo yamekuwa yakisumbua wananchi kwa kuwapora mali zao.

"Hatuhitaji kuwa na mazombi hapa," Waziri Mkuu aliagiza na kuzitaka kamati za mazingira katika vijiji vyote zihakikishe maeneo yote ya vyanzo vya maji yanalindwa na kuzuia shughuli za kibinadamu zikiwamo za kilimo, ufugaji na ukataji miti ili kuepusha taifa kugeuka jangwa.

Awali Mbunge wa Busanda, Tumaini Mageza alishukuru serikali kwa kuimarisha huduma za kijamii katika jimbo lao ikiwamo upatikanaji majisafi na salama. Hadi sasa tayari nyumba zaidi ya 200 zimeshaunganishiwa maji na vituo 10 vya kuchotea maji vimeanzishwa.

Mbunge huyo alitumia fursa hiyo kuomba serikali ianzishe mradi wa ujenzi wa shule za msingi za ghorofa kwa kuwa katika mji huo wanazaliwa watoto wengi, wakiwa na wastani wa watoto 1,000 kwa mwezi, hivyo wakiendelea kujenga shule za kawaida watakosa maeneo ya miradi hiyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Bil. 30/- kutumika kuimarisha huduma watoto wachanga

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

SERIKALI imesema katika mwaka wa fedha 2024/25 itatumia Sh. bilioni 30 kuimarisha huduma za watoto wachanga katika hospitali 100.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Stella Fiyao, aliyetaka kujua kama kuna mpango wa serikali kupeleka mashine za watoto njiti katika hospitali zote za mikoa na wilaya nchini.

Dk. Mollel alisema katika mwaka huu wa fedha serikali imepeleka vifaa vya kusaidia watoto njiti kwenye vituo vya kutolea huduma za afya 241 vyenye jumla ya thamani ya Sh. bilioni 2.6 hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu.

"Katika kipindi cha mwaka 2024/25, serikali imepanga kutumia Sh. bilioni 30 kwa ajili ya kuimarisha huduma za watoto wachanga katika hospitali 100 kwa kujenga wodi maalum (NCU) za watoto wachanga, watoto njiti na ununuzi na usambazaji vifaa tiba ikiwamo mashine za kusaidia watoto wachanga njiti kupumua," alisema Dk. Mollel.

Serikali pia imepanga kutoa ruzuku kwa mitungi ya gesi 452,445 yenye thamani ya Sh. bilioni 10 ili kuhakikisha bei ya nishati safi ya kupikia inapungua na kufikia lengo la asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ifikapo mwaka 2033/34.

Naibu Waziri wa Nishati, Judith Kapinga aliyasema hayo bungeni jana wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Lugangira.

Mbunge huyo alitaka kama serikali haioni haja ya kupunguza gharama ya gesi ili kufikia lengo la asilimia 80 ya Watanzania wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2033/34.

Naibu Waziri Judith alisema serikali inafanya jitihada kuhakikisha bei ya nishati safi ya kupikia inapungua.

Alisema kuwa kwa upande wa mitungi ya gesi inayopatikana kutoka kwenye viwanda vya kusafisha mafuta, ruzuku imetolewa kwa mitungi 83,500 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.5. "Katika mwaka wa fedha 2024/25, serikali itatoa ruzuku kwa mitungi 452,445 yenye thamani ya Sh. bilioni 10. Kwa upande wa gesi asilia, serikali inaendelea na uwekezaji wa ujenzi wa mabomba ya kusafirisha na kusambaza gesi majumbani.

"Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi ina mpango wa kuongeza miundombinu ili kupokea meli kubwa za gesi ya LPG na hivyo kushusha gharama za bidhaa hiyo," alisema Kapinga.

Naibu Waziri Judith alisema serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi zinazojihusisha na usambazaji na uuzaji gesi ya LPG na gesi asilia pamoja na kuwekeza katika ujenzi wa vituo vya kujaza gesi vinavyohamishika na visivyohamishika kwa kila wilaya.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi, Wilaya ya Kinondoni, Shaweji Mkumbula, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Tawi la Tegeta uliofanyika Dar es Salaam juzi ikiwa ni pamoja na kuwapokea wanachama wapya 15 waliohamia kutoka vyama mbalimbali vya upinzani. **PICHA: IMANI NATHANIEL**






# TARI yafanya utafiti wa kilimo mpunga unaostahimili mafuriko

**Na Jenifer Gilla**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) inafanya utafiti wa mbegu za mpunga zinazostahimili mafuriko ili kuepusha wakulima na hasara zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi.

Pia inasajili mbegu za mimea ya asili na kuziweka katika maduka ya mbegu za kilimo ili wakulima wanaohitaji wazipate kwa urahisi tofauti na sasa ambapo zinapatikana mbegu za kisasa tu.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Thomas Bwana aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa Kongamano la Wadau wa Mazingira, jijini Dar es Salaam, mgeni rasmi akiwa Makamu wa Rais, Dk. Phillip Mpango.

Alisema kwa sasa wapo katika hatua ya kukusanya taarifa kwa kupita katika mashamba yaliyoathiriwa na mafuriko na kukusanya sampuli ya mpunga uliostahimili kwa ajili ya kuchunguza vinasaba.

"Tunajiuliza kwa nini ule umebaki? Una vinasaba ambavyo vitatusaidia kujua kwamba huko mbele tutapata zao ambalo hata mafuriko yakiwapo litaendelea kustawi," alisema Dk. Bwana.

Alisema pia wanaboresha vinasaba kwenye mbegu za mazao ili kuongeza ustahamilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kuzalisha mbegu zinazotoa mazao kwa muda mfupi na zile zinazostahimili ukame.

Pamoja na hilo, taasisi hiyo pia inafanya utafiti na kuhamasisha kilimo cha mpunga kinachotumia maji kidogo ili hata kukitokea ukame wakulima waendelee kuzalisha zao hilo.

Dk. Bwana alisema kutokana kuwapo uhitaji wa mbegu za asili, wameanza utaratibu wa kuzalisha mbegu hizo na baada ya muda zitasambazwa katika maduka ya mbegu za kilimo ili mkulima anayezihitaji azipate.

Alisema kilimo kinaathirika kwa kiasi kikubwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira, hivyo kunahitajika uwekezaji mkubwa kwenye utafiti ili kuiokoa nchi na janga la njaa.

Alisema kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) wanatoa ushauri kwa wakulima aina gani ya mazao wapande kulingana na hali ya hewa tarajiwa ili kuepuka hasara.

Mkuu wa Kitengo cha Utafiti na Mazingira, Dk. Sara Osima, alisema taasisi hiyo imeboresha miundombinu ya kufanyia kazi ili kutoa taarifa sahihi za hali ya hewa katika muda sahihi ili kuepuka athari zitokanazo na mabadiliko ya hali ya hewa.

Alisema pia wameboresha kitengo cha mawasiliano kwa umma ambao wanatumia miundombinu ya kisasa pamoja na kushirikiana na vyombo vya habari kutoa taarifa za hali ya hewa kwa wananchi.

Mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), Dk. Deo Shirima, alisema katika kuhakikisha wanaboresha uzalishaji chakula nchini wameweka vituo zaidi ya 20 nchini vinavyofanya kazi kwa ukaribu na wakulima.

Vituo hivyo pia vinajifunza changamoto wanazopitia wakulima katika maeneo hayo na kuzitafutia suluhisho ikiwamo kuwapelekea teknolojia ya kilimo cha kisasa kinachohimili athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Meneja wa Utafiti wa Mazingira wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Rose Mtui, alisema baraza hilo linajikita kutekeleza sheria za mazingira ili kuhakikisha yanalindwa.

Alisema pia wana jukumu la kufanya utafiti juu ya hali ya mazingira ya bahari na nchi kazi na kutoa machapisho ili jamii na wadau wafahamu hali halisi ilivyo na watafute suluhisho.



# Wafugaji sasa wamwangukia Rais Samia

**Na Jaliwason Jasson,** KITETO

WAFUGAJI wa Kijiji cha Irkishibor wilayani hapa Mkoa wa Manyara, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutatua mgogoro wa mpaka baina yao na Pori la Akiba la Mkungunero ili kuruhusu shughuli za kiuchumi na hifadhi kuendelea.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho, wanawatuhumu askari wa pori hilo, kuwanyanyasa, kukamata ng'ombe zao na kuvunja maboma 88 yaliyokuwa na kaya 2,856 zenye watu 5,000.

Kwa nyakati tofauti jana, wakazi hao akiwamo Julius Simon alisema kuwa: "Tunaomba Rais asikie kilio chetu, aje aone na kutusikiliza tunavyonyanyaswa na kuondolewa kwa makazi yetu ya kudumu na Pori la Akiba la Mkungunero."

Alisema katika eneo hilo vimeharibiwa visima vya maji vya asili 22 vilivyokuwa vinahudumia mifugo katika vitongoji vitano vya kijiji hicho.

James Satuli, ambaye ni kiongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai (Laigwanani), alisema mwaka 2018, askari hao, walikamata ng'ombe wake 311.

"Wale ng'ombe waliishia kule Kondoa (Dodoma) na ndama 73 waliokuwa wamebaki nyumbani walifia palepale kwa kukosa maziwa," alisema Satuli.

Kiongozi huyo wa kimila, alisema licha ya kushtakiwa na mahakama kuamuru warejeshewe mifugo yao, mpaka sasa amri hiyo imepuuzwa.

Jackson Ole Kau, alisema tatizo lililoko ni mwingiliano wa mipaka na kwamba wanaendelea kunyanyaswa na askari wa pori hilo.

Kau, alisema aliwahi kuufikisha mgogoro baina yao na pori hilo bungeni kwa Waziri wa Maliasili na Utalii wa wakati huo, Ezekiel Maige.

Masinyali Meshaki, alisema Mkungunero imekuwa tishio kwao kwa kuwakosesha amani, hivyo wanamwomba Rais Samia kuingilia kati kwa kutatua.

Mhifadhi Mkuu wa Pori hilo, Flora Kalambo, alisema kwa sasa hawana mgogoro na wanakijiji hao.

Kalambo, alisema awali mgogoro ulikuwapo kuanzia mwaka 1996 kutokana na mwingiliano wa mipaka wa vijiji vya Kimotoloko, Irkishibor na Lobosilet vya Mkoa wa Manyara.

Alisema vijiji hivyo vilipimwa na kuingia Mkoa wa Dodoma kwenye pori hilo.

Pia, alisema mwaka 2019, mgogoro huo ulitolewa maelekezo na serikali na mwaka 2022 walianza kutekeleza maelekezo ya Baraza la Mawaziri.

Kalambo, alisema serikali iliwataka kufanya uthamini kwa vijiji vya Dodoma na kuwalipa fidia wananchi waliokuwa na maboma kwenye pori hilo 158.

"Tumeishalipa fidia wananchi 125, bado 33 ambao walikuwa na matatizo ya kukosa akaunti za benki, kukosa Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na matatizo ya mirathi," alisema.

Kuhusu Mkoa wa Manyara, alisema katika Kijiji cha Kimotoloko walibaini maboma 39 na baada ya kutafsiriwa mipaka ikagundulika wapo Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma, hivyo walitakiwa kumega eneo la kijiji hicho ekari 558 kutoka Mkungunero ili kuwahamisha.

Alisema kwa Kijiji cha Irkishibor baada ya kufanya tathmini Mkungunero ilitakiwa kumega ekari 11,891 zirejeshwe kwa wananchi.

Eneo hilo alieleza kuwa kulikuwepo vitongoji vya Lombenek, Imbopom na Elichura ambavyo baada ya kumega viwili vilibaki Kiteto isipokuwa Kijiji cha Elichura kipo ndani ya hifadhi upande wa Wilaya ya Kondoa.

# Wazazi CCM kujenga viwanda nchini

**Na Steven William,** MUHEZA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa imetangaza mpango wa kuanzisha mradi wa ujenzi wa viwanda katika mikoa mbalimbali ya nchini ili kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana.

Mpango huo ulitangazwa na Mwenyekiti wake, Fadhil Maganya baada ya kukagua Shule ya Sekondari ya Wazazi iliyopo Mbaramo wilayani hapa Mkoa wa Tanga mwishoni mwa wiki iliyopita.

Akizungumza katika shule hiyo inayomilikiwa na jumuiya hiyo baada ya kusimama kutoa huduma kwa muda mrefu na kukagua ujenzi wa nyumba mpya ya Katibu wa Wazazi wilaya, Maganya, alisisitiza wamejipanga kuanzisha ujenzi wa viwanda nchini.

Alisema katika mpango huo, Muheza watajenga kiwanda cha kusindika maji ya matunda ya machungwa katika eneo la Kwafungo kwenye eneo lenye ukubwa wa hekari 50.

Alisema wanampango kujenga kiwanda kingine cha nguo katika Wilaya ya Bunda mkoani Mara, kiwanda cha vifaa tiba mkoani Dodoma, Kahama (Shinyanga), Iringa, Pemba na hospitali ya rufaa ngazi ya mkoa na ujenzi wa mradi wa Benki ya Jumuiya ya Wazazi.

Akizungumza katika mikutano yake mji wa Mombo, Korogwe, Muheza na Tanga mjini, alisema jumuiya hiyo inamiliki miradi ya shule za sekondari takribani 70 nchini na vyuo viwili.

Alisema katika shule hizo, 30 zimejifunga kutokana na kutofanya kazi na 40 zinaendelea kutoa elimu kwa wanafunzi na walizoingia nazo ubia kwa wawekezaji 18.

Mwenyekiti wa Wazazi Muheza, Hatibu Bakari, alisema kwa wilaya hiyo, wamejipanga kuhakikisha mradi wa sekondari ya wazazi unaanza upya baada ya kupata mwekezaji mpya wa kuifufua.

Kwa mujibu wa Bakari, jumuiya hiyo kwa wilaya ya Muhezawanataka kuona uwekezaji mkubwa wa kiwanda cha kusindika maji ya matunda ya machungwa kinatoa ajira kwa vijana baada ya uzalishaji kuanza.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC**, tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MOSHI | INNOCENT APOLINARY MALLYA | NYUMBA | INNOCENT APOLINARY MALLYA | MSARANGA MOSHI | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | JULIUS STANLEY MALLYA | NYUMBA | JULIUS STANLEY MALLYA | BOMANG'OMBE HAI | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | NYUMBA | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | BOMANG'OMBE HAI | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SCOLASTICA SIRILY TEMBA | NYUMBA | PAUL ELVIS NGOWI | KARIKACHA- MOSHI | 19/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | CHEGE REUBEN OGILLO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | CHEGE REUBEN OGILLO | MSARANGA MOSHI | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | ALEX SABAS SILAYO | NYUMBA | ALEX SABAS SILAYO | MABOGINI-MJOHORONI MOSHI | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI- MSAKUZI | 12/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | STEWART EDSON MWANGALABA | SHAMBA | STEWART EDSON MWANGALABA | MKURANGA | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | IPYANA GIDEON TUNTUFYE | NYUMBA | IPYANA GIDEON TUNTUFYE | KIMARA 'B" | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELYKWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA- MISSION | 12/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | YOHANA BRUNO SHAYO | NYUMBA | WILSON ELICHILIA MBOYA | BOKO | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | MUSSA MATHIAS SHIJA | NYUMBA | MUSSA MATHIAS SHIJA | UDINDIVU,MAPINGA | 17/06/2024 SAA 7:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | PADONI KIBAYU SIMON | NYUMBA | PADONI KIBAYU SIMON | PUGU- VIWEGE | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | JACQUELINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | SABATO DAVID OKUKU | MIKWAMBE- TOANGOMA | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JOYCE MARIJANI MSOFFE | NYUMBA | JOYCE MARIJANI MSOFFE | KIMARA | 15/06/2024 kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | NYUMBA | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | YOMBO VITUKA | 19/06/2024 kuanzia saa 4 asubuhi na kuendelea |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 14/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | OSCAR JACKSON SEME | NYUMBA | OSCAR JACKSON SEME | MBEZI- MSAKUZI | 12/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | ELISANTE BERNAD MRTA | NYUMBA | ELISANTE BERNAD MRTA | KIGAMBONI | 14/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | DICKSON CHRISTIAN NGEMELA | NYUMBA | DICKSON C. NGEMELA | KIMARA | 12/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | NYUMBA | EDNA ISHENGOMA RWEMILINZI | TEGETA "A" | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | NEEMA FELIX MSIMAMI | NYUMBA | NEEMA FELIX MSIMAMI | LUGWADU MKOKOZI | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGEA | FATUMA BAKARI BENDERA | NYUMBA | FATUMA BAKARI BENDERA | VIKAWE | 21/06/2024SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 21/06/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | JUMA NURU MUSHI | NYUMBA | JUMA NURU MUSHI | MBAGALA | 14/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1002975 KIWANJA NA. 2483, KITALU 'A' MBEZI MANYEMA 2.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 3. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA NYANDOTO 2.SALUM JUMA MARWA 3.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.MBEZI MANYEMA 2.KIGOGO KATI 3.KINZUDI GOBA | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI-MWANZA | 17/06/2024 SAA 12:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 18/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 20/06/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 17/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 20/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI | 21/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | HELENA ANTONY HALENGO | NYUMBA | MARIA ANTHONI SKAWEWE | ILEMI | 21/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | MARIAM BATON MWANDENENE | NYUMBA | VUMILIA ELIAS NYAGAWA | NGOSI-MWAKIBETE | 25/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | FELIX MAVIKE MSIGWA | NYUMBA | FELIX MAVIKE MSIGWA | ILEMI | 21/06/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA |
| MBEYA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | NYUMBA | YESAYA SAMWEL KIBONDE | TEMBELA | 24/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBEYA | EMANUEL MOYO MASETA | 1.NYUMBA (3) (2) KIWANJA | EMANUEL MOYO MASETA | 1. IFWEKENYE MBEYA 2.SONGWE | 25/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | CHARLES SIMON MALOMELE | NYUMBA | CHARLES SIMON MALOMELE | NDACHI-DODOMA | 18/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0715868000/0714939933/0785242219/0759282344/0787129539/0767808848/0754497396/0678799566/0655715138/0759648448
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



# TDB yaagizwa kubadili vifungashio vya maziwa

**Na Elizabeth Faustine,** MWANZA

SERIKALI imeiagiza Bodi ya Maziwa nchini (TDB) kufanya mabadiliko ya vifungashio vya maziwa ili kupunguza bei ya maziwa nchini.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti wakati akifunga Maadhimisho ya 27 ya Wiki ya Maziwa Duniani yaliyofanyika kitaifa jijini Mwanza.

Mnyeti, alisema bei ya maziwa ipo juu hali inayosababisha wananchi kushindwa kumudu, hivyo kuongeza hali ya udumavu kwa watoto nchini kutokana na bei ya vifungashio vya nailoni kuwa ghali.

"Kaeni muone namna ya kutumia rasilimali za mbao kutengeneza vifungashio badala ya nailoni zinazotumika sasa ili kupunguza bei ya maziwa," alisema Mnyeti.

Alisema licha ya serikali kugawa mbegu bora za ng'ombe, bado Watanzania hawana utamaduni wa kunywa maziwa kutokana na kinywaji hicho kuonekana kama anasa kutokana na gharama zake.

Mwenyekiti wa Bodi ya Washauri wa TDB, Profesa Zakaria Masanyiwa alisema kuwa katika siku tano za maadhimisho hayo, wadau wamepata fursa ya kujifunza, kupata elimu na ujuzi kuhusiana na tasnia ya maziwa.

Manyiwa alitoa wito kwa wananchi kutumia elimu hiyo kwa ajili ya maendeleo ya tasnia hiyo ya maziwa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Daniel Mushi, alisema wameanza kushughulikia changamoto zinazoikabili tasnia hiyo ikiwemo kuhamasisha vijana katika uzalishaji wa maziwa na kudhibiti bei za maziwa nchini.

# Mtendaji ajinasua jela kwa rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita imemhukumu Ofisa Mtendaji wa Kata ya Nyamwilolewa, Simon Maduka Jeseph (34) kulipa faini ya Sh. 500,000 kwa kupokea rushwa ya Sh. milioni 1 kutoka kwa Pili Mwanzalima ili asimchukulie hatua kwa kumhifadhi mhamiaji haramu nyumbani kwake.

Mshtakiwa huyo alilipa faini hiyo na kunusurika kwenda jela miaka mitatu katika hukumu ilitolewa hivi karibuni na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Cleofas Waane, baada ya upande wa mashtaka kuthibitisha pasipo kuacha shaka kuwa mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo.

Hakimu Waane alisema kuwa mahakama hiyo inatoa adhabu kali dhidi ya mshtakiwa huyo ya kutumia kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini hiyo ili iwe fundisho kwake na kwa maofisa watendaji wa kata wengine wenye tabia kama yake.

Alisema kuwa: "Mahakama hii inakutia hatiani mshtakiwa kwa kosa ulilioshtakiwa nalo, na inakutaka utoe maombolezo ili iweze kukupunguzia adhabu.

Wakili wa mshtakiwa huyo, Daudi Mhagama, aliiomba mahakama hiyo imsamehe mteja wake huyo kwa madai kuwa mkosaji wa mara ya kwanza, mama yake ni mgonjwa na familia yake inamtegemea, hivyo anaomba mahakama impunguzie adhabu.

Hakimu huyo alitupilia mbali utetezi huo na kumhukumu mshtakiwa huyo.

Awali Wakili wa Serikali, Kabura Benjamin, alidai kuwa hana kumbukumbu za makosa ya nyuma ya mshtakiwa, hivyo anaiomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka iliyosomwa na Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Antidius Rutayuga, Aprili 4, mwaka jana mshtakiwa huyo alipokea kiasi hicho cha fedha ofisini kwake kutoka kwa Pili Mwanzalima ili asimchukulie hatua kwa kosa la kumhifadhi mhamiaji haramu aliyejulikana kwa jina moja la Amos nyumbani kwake, kinyume na sheria.


## TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**TWINS AUCTION MART COMPANY LIMITED,** kwa idhini na mamlaka tuliyo pewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali/dhamana za mdaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya notisi/Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALA DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | GODFREY THOMAS KIMATH | GODFREY THOMAS KIMATH | NYUMBA | VIKINDU, WILAYA YA MKURANGA, MKOA WA PWANI | 19/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 2 | ALEX MTUNDU MIHUMHA | ALEX MTUNDU MIHUMHA | NYUMBA | KIPUNGUNI 'B' KITUNDA MANISPAA YA ILALA | 22/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3 | ANNA J. ISACK | SALUM IBRAHIM MAGIMBA | NYUMBA | YOMBO DOVYA, MAKANGARAWE MANISPAA YA TEMEKE | 25/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| | | MTUNDA RAMADHANI SELEMANI | NYUMBA | MCHIKICHINI, KIBONDEMAJI MANISPAA YA TEMEKE | 25/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4 | KADEWELE SALUM OMARI | KADEWELE SALUM OMARI | NYUMBA | MWEMBE MADAFU, UKONGA MANISPAA YA ILALA | 27/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5 | CHARLES YUSUF PUKA | GASPAR WILLIAM MWAKANYAMALE | NYUMBA | PUGU MWAKANGA MANISPAA YA ILALA | 29/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| | | CHARLES YUSUF PUKA | NYUMBA | MJI MPYA, MAJOHE MANISPAA YA ILALA | 29/06/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 6 | SETI Z. ERNEST | SETH ERNEST ZAKARIA | NYUMBA | VIWEGE 'B', MAJOHE MANISPAA YA ILALA | 03/07/2024 KUANZIA SAA 10:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyo fikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

**TWINS ACTION MART COMPANY LIMITED**
**P.O.BOX 1305, Songea, Ruvuma**
**Tel: 0757 940 064/ 0716 070 298/ 0784 718 734**
**Email:twinscoltd5@gmail. com**


# Ujenzi tawi la UDSM Bukoba mbioni

**Na Restuta Damian,** KAGERA

SERIKALI mkoani hapa imemkabidhi mkandarasi eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika Kijiji cha Itawa Kata Karabagaine Wilaya ya Bukoba.

Akikabidhi eneo hilo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Fatma Mwasa, alisema kuwa ujenzi wa chuo hicho utakuwa sehemu ya fursa ya kukuza uchumi na ongezeko la elimu kwa wakazi na wageni kutoka maeneo ya ndani na nje ya nchi.

Mwassa, alisema dhamira ya serikali ni kuona wanafunzi wanajitahidi katika masomo yao shuleni ili kuifikia elimu ya juu.

Alisema ndiyo sababu elimu hiyo ya juu imesongezwa mkoani hapa ili kutoa fursa kwa vijana wengi kuendelea na masomo badala ya kuishia kidato cha sita.

Alimtaka mkandarasi hiyo kuhakikisha ujenzi wa miundombinu ya majengo ya chuo hicho inaambatana na ya maji na barabara na kukamilika haraka.

Makamu Mkuu wa UDSM, Profesa Bonventure Rutinwa, alisema ujenzi wa chuo hicho unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh.bilioni 20.

Kwa mujibu wa Profesa Rutinwa, mkataba wa ujenzi wa chuo hicho ambao unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi 18, ulisaniwa Mei 17, mwaka huu.

Alitaja kozi ambayo zitatolewa katika chuo hicho kuwa ni za biashara, uchumi wa kimataifa na kutakuwa na kituo cha mafunzo ya ujasiriamali kwa kila mwananchi..

# Wafanyabiashara, TRA wayajenga

**Na Alex Sayi,** MASWA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) wilayani hapa Mkoa wa Simiyu imekutana na wafanyabiashara kujadili njia rahisi ya kulipa kodi kwa hiari.

Akizungumza juzi wakati wa kikao hicho, Meneja wa TRA wa Wilaya ya Maswa, Lucius Theonest, alisema kuwa wamefikia hatua hiyo baada ya kubaini baadhi ya wafanyabiashara hawalipi kodi hadi nguvu za ziada zitumike.

Theonet, aliwataka wafanyabiashara hao kujenga mazoea ya kulipa kodi kwa hiari na kuhakikisha wanatumia mashine za EFD, kutunza kumbukumbu za manunuzi na mauzo ili iwe rahisi kufanyiwa makadirio na mamlaka hiyo.

Alisema ofisi yake inaendelea kuhakiki mizigo ya wafanyabiashara inayoingizwa wilayani hapa kutoka mikoani ili kuhakikisha imelipiwa kodi.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya hiyo, Aswege Kaminyoge, aliwataka wafanyabiashara hao kujenga mazoea ya kukutana na serikali na kuwasilisha kero zao.

Baadhi ya wafanyabiashara hao, akiwamo John Chagu, walisema baadhi ya maofisa wa TRA wamekuwa hawawashirikishi wakati wa kufanya makadirio ya kodi na kusababisha kutozwa kiwango kikubwa cha fedha.

Nipashe
# TESA
Jumanne Juni 4, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI





Ukurasa 14



Ukurasa 12

'Tunza miti, tupa shoka kulinda misitu, anza kuweka mizinga'



Ukurasa 13

MKOA HATARINI NJAA
'Makahaba' wajaa mashambani wakiwinda mazao, hubadilishana kwa ngono

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# GOOGLE mtaalamu anayekujuza kila kitu lakini ukimwendekeza ...




GOOGLE wengi huitamka 'gugo' lakini kwa usahihi inatamkwa 'gugil' zama hizi ndiyo maktaba inayohifadhi taarifa zote. Inakupa kila kitu unachokihitaji kwa wakati huohuo, haipotezi muda.

Ukitaka taarifa za maswali darasani, maafa yaliyotokea popote, maana za maneno, aina za vitu, elimu ya afya na maradhi yanayokusumbua maktaba hiyo itakujibu.

Mathalani, zamani ungeweza kwenda hospitalini ukachunguzwa kikafahamike kinachokutafuna lakini usijue una shida gani ni kwa sababu huelewi lugha inayotumiwa na daktari kuandika taarifa za ugonjwa wako wala dawa anazokupa.

Leo, mambo yamebadilika kila kitu unachoandikiwa au kukisikia iwe kuhusu maradhi, tiba, biashara na chochote unachohitaji unaangalia kwenye gugo.

Kwa hakika inaogopesha kwa kuwa ina taarifa nyingi na inajua kile ambacho unakitafuta na inakuelekeza mahali pa kubofya. Katika kompyuta au simu, Google imehifadhi chochote unachotaka, haihitaji kupewa muda wala kuulizwa mara mbili.

Mojawapo ya shida kuu za kusaka taarifa na kupata utambuzi wa mambo yanayowasumbua watu mtandaoni ni taarifa za afya au magonjwa. Mfano, ukiwa na dalili fulani unakimbilia kwanza kuzitafuta kwenye Google huo ndiyo msaada halisi wengi wanaouamini.

Kwa mfano, mtu anayejihisi kuumwa shingoni na uvimbe anaiuliza gugo itambue ugonjwa wake na anapopata baadhi ya dalili wasiwasi unaongezeka kulingana na maelezo kutoka mtandaoni.

Anaanza na mtandao kabla ya kukutana na mtaalamu wa afya kutatua tatizo lake. Kila kitu, hasa maradhi yanayowasumbua watu uchunguzi huanzia gugo, akiaminika kuwa mtaalamu anayejua ni tatizo gani na dawa zipi zinaweza kusaidia shida kwa haraka kabla ya kugonga hodi hospitali.

Kumbuka kutokana na umuhimu wa kujua ukweli na kuchunguza afya gugo inapokupa taarifa potofu kwenye mtandao, unaweza kuchanganyikiwa na ukawa na hofu zaidi ya kile kinachokuuma.

Mfano ukaona maneno machache na kuanza kufikiria kuwa una shida kubwa. Mathalani ukiangalia kwenye gugo sababu za kuumwa kichwa usiku kila unapoamka na mwili kulegea unaweza kuona mwisho wa maisha yako umekaribia.

Mtandao utakujibu kuwa ni dalili za kuwa uvimbe kichwani, kukandamizwa mishipa ya fahamu ya shingo na ubongo kunakoweza kukusababishia kiharusi au kupooza upande mmoja.

Taarifa hizo zinaweza kukuchanganya na kukuvuruga kumbe ni mambo ambayo hayakuwa sahihi na unapobofya au'click' eneo hilo haimaanishi kuwa ndiyo shida uliyo nayo, pengine tatizo lako ni kukosa usingizi au hewa safi chumbani.

Inawezekana una dalili zinazohusiana na hayo uliyoyaona kwenye gugo lakini kwanza cha kufanya ni kuachana na vyanzo visivyoaminika, ambavyo vinaweza kusababisha hofu zaidi na zaidi ukipata 'presha'.

Kumbuka gugo siyo chanzo cha kuaminika cha kila kitu hivyo 'usijinyonge bure' kisa umeona kuumwa kichwa ni dalili za kuwa na uviumbe kichwani ukaanza kuhofu kuwa utafanyiwa upasuaji wa kichwa na kuguswa ubongo, yote hayo yakikuongezea hofu mara dufu. Kikubwa nenda hospitalini pima ili kujua ukweli wa mambo.

Watu wakumbuke kuwa 'sisi' siyo wataalamu wa afya au madaktari, hakuna sababu ya kujitambua au kujigundulia ugonjwa ambao huna, au mbaya zaidi, kujitibu wakati hata hajui ni nini kinaendelea mwilini mwako.

Tatizo lolote linahitaji uangalizi wa kitaalamu, iwe ni kwa njia ya matibabu au kufanya uchunguzi, taarifa za mtandaoni wakati mwingine siyo za ukweli, dawa zilizopendekezwa pia zaweza kuwa si sahihi.

Hupaswi kujaribu kununua dawa kisa umeona jibu mtandaoni linalohusiana na dalili za tatizo ulilolona kwenye gugo njia pekee salama ya kupata tiba inabaki kuwa kwa daktari atakayekuchunguza na kukupa dawa.

Kama ukiona kuna kitu hukielewi muulize daktari vipimo hivi maana yake ni nini? Ukiona ameandika ripoti ya maradhi ya yako uliza anaamanisha nini?

Sio kwamba ni jambo baya kufuata taarifa kwenye gugo lakini unaweza kuogopa kupita kiasi kutokana na kile unachosoma au kutotafuta msaada. Mtandaoni si pabaya lakini ni vyema kuacha utambuzi ufanywe na wataalamu kwa faida yako.

Kuna watu walio na wasiwasi wa kiafya ambao mara nyingi huamini kuwa wana jambo baya au maradhi ya kutisha hawa wana uwezekano mkubwa wa 'kugugo' dalili za tatizo au wanachokiona kimeandikwa kinaweza kuongeza hofu na hatari zaidi wakati wa kudhani kuwa wana maradhi fulani.

Mfano wako baadhi ya watu wakiona vifupisho vinavyo-

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA DK. FELICIAN B. KILAHAMA

# ‘Tunza miti, tupa shoka kulinda misitu, anza kuweka mizinga’




Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, akikabidhiwa tuzo na Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki , kutambua mchango wa Rais Samia Suluhu Hassan, kuendeleza sekta ya ufugaji wa nyuki na uhifadhi wa mazingira. **PICHA: MTANDAO**

UFUGAJI nyuki ni shughuli ya kiuchumi inayoajiri Watanzania zaidi ya 2,000,000, jambo linalopaswa kuwa kichocheo cha kuwatunza nyuki viumbe, rafiki wa binadamu na mazingira.

“Tanzania kuna wafugaji nyuki, pamoja na wauzaji mazao ya nyuki, wenye viwanda vya kuchakata mazao ya nyuki na wasambaji zaidi ya 2,000,000. Hivyo, nyuki ni rasilimali muhimu kwa kuzingatia kuwa ni chanzo cha ajira kwa wengi.”

Anasema Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Sinyamule na kuongeza: “Ni lazima kutunza mazingira ili kuwawezesha nyuki kuendelea kuwepo kwa wingi kwa faida ya taifa. Acha shoka kukata miti anza kutundika mizinga”.

Anayasema hayo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Nyuki Duniani, inayofanyika kitaifa mkoani Dodoma.

Nyuki ni muhimu kwa wanadamu na mazingira , ndiyo maana Umoja wa Mataifa (UN), Disemba, 2017; unapitisha azimio la kuadhimisha siku ya Nyuki Duniani, kila ifikapo Mei 20.

Ni uamuzi unaokwenda sambamba na Azimio la Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) la mwaka 2015, lililokuwa na maudhui hayo.

Tanzania inaadhimisha siku ya nyuki duniani na mwaka huu ilikuwa Dodoma, na Dk. Philip Mpango, Makamu wa Rais, akiwa mgeni rasmi.

Dodoma ilitikisika zikijaa shamrashamra za ainayake kuonyesha umuhimu wa nyuki katika maisha ya binadamu na sekta ya mazingira.

Maadhimisho hayo yaliambatana na onyesho la shughuli zinazofanywa na wajasiriamali pamoja na wadau wengine wanaojihusisha na biashara ya mazao ya nyuki.

Hivyo, kwa mwaka 2024, wajasiriamali na wadau takribani 90 wanashiriki kikamilifu wakionyesha mazao na bidhaa mbalimbali kutokana na kazi nzuri inayofanywa na ‘nyuki’.

Ilikuwapo asali ya nyuki wanaouma na wasiouma, nta, chavua inayokusanywa na nyuki wakati wa kutafuta malighafi ya kujitengenezea chakula chao na malikia.

Katika harakati hizo, nyuki hutembelea maua mengi na kukusanya chavua ya kutosheleza mahitaji yao lakini binadamu, pia huchukua sehemu ya chavua waliyoipata kabla hawajaingia kwenye mizinga ili kutengeneza asali ambayo pia binadamu hufaidi.

Washiriki mbalimbali walikuwepo wakiwamo wanafunzi wa Shule ya Msingi Mvomero ya mkoani Morogoro inayowakilishwa na washiriki watatu wa darasa la nne, la sita na la saba.

Hawa walitoka kwenye shule ambazo zimejiunga na programu jumuishi ya ‘eco-schools’ inayoendeshwa na shirika la kutunza na kuendeleza misitu nchini la ‘Tanzania Forest Conservation Group’ (TFCG), la Dar Es Salaam, kwa ufadhili wa Serikali ya Denmark.

Wengine ni Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) na ‘Kijiji cha Nyuki Co Ltd’ kutoka Singida.

Kwa Tanzania ni adhimisho la tano tangu UN kuiweka Mei 20, kuwa siku maalumu kwa mataifa kuadhimisha na kuudhihirisha umuhimu wa viumbe nyuki katika mustakabali wa maisha ya wanadamu na jinsi wanavyosaidia kuyaboresha kupitia mazao mbalimbali.

Kaulimbiu kwa mwaka huu, ilikuwa ni: “Nyuki kwa Afya na Maendeleo: Tuwatunze”. Kiini cha kaulimbiu hiyo ni kuonyesha jinsi gani nyuki ni rafiki wa binadamu au ni kuwahakikishia Watanzania kuwa uwepo wa viumbe hao ni muhimu kwa afya zao .

Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Hassan Abbas, anakumbusha kuwa Mohamed Ali, sasa (marehemu) alijulikana kuwa ni mfalme wa ngumi duniani, wakati wa uhai wake aliwahi kusema “elea kama kipepeo na au dunga kama nyuki.

Kwa usemi huo, alionyesha kuwa nyuki siyo wa kuchezewa hovyo maana ni kiumbe hatari kwa wanaofanyia yasiyotakiwa.

Lakini, pia usemi huo ukionyesha jinsi Ali alivyokuwa wa kuogopwa kwa kudunga ngumi moja inayoangusha chini mpinzani wake.

Dk. Abbas anaeleza kuwa hata zama za kale, umuhimu wa nyuki kwa uhai wa binadamu ulijulikana.

Anafafanua kuwa umuhimu wa nyuki umedhihirishwa ipasavyo kwenye vitabu vya dini zote.

Makamu wa Rais, Dk. Mpango, akizindua Siku ya Nyuki Duniani, anasema: “Wakati wa kuiandaa hotuba ya kuadhimisha siku hii muhimu duniani, sikujaliwa kupata jina zuri na sahihi linaloonyesha umuhimu wa ‘nyuki’ kwa maisha ya binadamu.

Wataalamu wa masuala ya ‘nyuki’ na baiolojia eti wanaita ‘mdudu nyuki’. Kusema kweli, hili siyo jina zuri kwa viumbe ambao ni wenye umuhimu sana wa kuwaletea binadamu faida kubwa”.

Anaonyesha nia ya kupata jina zuri la Kiswahili litakalowatambulisha na kuonyesha kiuhalisia na umuhimu wao kwa afya za wanadamu na maendeleo ya taifa.

Kadhalika, anasisitiza umuhimu wa nyuki katika kuimarisha uchumi wa taifa kupitia kuuza nje bidhaa zitokanazo na nyuki kupata fedha za kigeni.

Anaishauri Wizara ya Fedha kupunguza kodi na tozo kwenye vifaa vya kuchakata na vifungashi vya mazao ya nyuki.

Kadhalika, vyombo vya habari kuzidisha juhudi za kutoa elimu na kuhakikisha wahusika wanatembelea shule zenye mafunzo yanayolenga kulinda na kutunza vyema mazingira pamoja na ufugaji nyuki

Akiunga mkono juhudi za kila mdau, Makamu wa Rais, anasisitiza umuhimu wa kuwashirikisha wadau wengi kwenye matukio ya kitaifa kuhusiana na ufugaji wa nyuki na kusisitiza umuhimu wa sekta ndogo ya nyuki kuendelezwa kwa manufaa ya utalii wa ndani na nje, ulijitokeza.

Awali, Makamu wa Rais, anapotembelea wadau kadhaa wakiwamo wanafunzi wa shule ya msingi walio kwenye program ya eco-schools, UDOM na wajasiriamali wa ‘Kijiji cha Nyuki.

Anaelezwa kuwa wanafunzi wa UDOM kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) wametengeneza utaratibu wa kufuatilia nyuki kiidijitali.

Mbinu hiyo inafuatilia maendeleo ya uazalishaji asali katika mizinga bila ya kwenda kwenye eneo ilipotundikwa na kwamba teknolojia hiyo inaweza kutumiwa na wafugaji wengi, itakuwa na tija kwa mfugaji binafsi, jamii na taifa.

Aidha, katika maonyesho hayo, Mtendaji Mkuu wa Kijiji cha Nyuki Philemon Kiemi, anasema hutoa mafunzo kwa vitendo, kwa vijiji jirani na kutoka mahali pengine kwa wenye nia ya kufuga nyuki, kulingana na mahitaji.

Mafunzo huchukua mwezi, wakifunzwa namna ya kuanzisha mashamba ya nyuki, njia bora za kurina asali na kuvuna mazao mengine ya nyuki kama chavua, nta ,sumu, maziwa pamoja na kuchakata mvinyo utakanao na asali.

Anaongeza kuwa wafugaji wa nyuki wamezoea kuzalisha asali kwa kutumia mizinga ya jadi na hupata asali kidogo na kwamba huduma wanazozitoa zinalenga kuwawezesha wafuga nyuki Singida na maeneo ya jirani kufuga kisasa na kibiashara.

## GOOGLE MTAALAMU ANAYEKUJUZA KILA KITU LAKINI UKIMWENDEKEZA ...

**INATOKA UK.11**

tumiwa na madaktari vimeandikwa kwenye karatasi za matibabu kama PHM, BID, BD, DOA, CRF, CT na 4/52 hufuata tafsiri zake kwenye gugo ili kufahamu kilichoandikwa kwenye karatasi za matibabu. Si jambo baya lakini kumbuka hofu inaongezeka na hata kukata tamaa kunaweza kukunyemelea.

Ukweli ni kwamba pamoja na habari na taarifa nyingi zinazopatikana kiganjani kwenye simu yako au kompyuta, kwa mtu anayeumwa kuusaka sana ukweli juu ya tatizo lake ni kama kujiongezea zaidi wasiwasi wa kiafya iwapo hataweza kuhimili atakachokutana nacho.

Hata kama umeonana na daktari akakufanyia vipimo na kugundua tatizo lako kuujua ukweli zaidi kwenye gugo si jambo baya ila amini na chukua taarifa sahihi za daktari ili kuepuka kujiongezea matatizo.

Kwa kutumia ‘google’ kunakupa taarifa za kitu unachofikiria au kuhisi kuwa ndilo tatizo ulilo nalo mwilini lakini kuinaibua na mengine ambayo hukuwa na haja ya kuyafahamu.

Kuamini sana ‘gugo’ kunaweza kuongeza mhemko na wasiwasi kuhusu shida ya ugonjwa ambao mhusika anao na hata kukufanya uchanganyikiwe, pia kushusha kinga ya mwili.

ELIMU

**NA SHABAN NJIA, SHINYANGA**

MKOA HATARINI NJAA

# ‘Makahaba’ wajaa mashambani wakiwinda mazao, hubadilishana kwa ngono

MATATIZO ya malezi ya watoto na wanafunzi yanayochangia kukosa mahitaji muhimu hususani wasichana kunaendelea kusababisha wengi kuangukia kwenye vishawishi vya mapenzi hata kuishia kupata ujauzito, wakianza kulea mapema huku wakikatisha masomo.

Kila kukicha kumekuwa na kesi nyingi za watoto wa kike kuachishwa masomo kutokana na mimba au ndoa za ututoni, hali hii imekuwa mzigo kwa familia na taifa, jambo linalowaweka lawamani wazazi na walezi, kuwa ni walegevu.

Ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2023 inaeleza kuwa watoto walioathirika na uvunjaji wa haki zao ikiwamo kupata ujauzito ni asilimia 45, wanawake asilimia 30, wanaume asilimia 10 na wazee asilimia 12.

Katika Kata ya Mwamala Wilaya ya Shinyanga wananchi huzalisha mazao mengi ya chakula na biashara na kipindi cha mavuno wanaume wanatuhumiwa kuhonga mavuno kwa wanawake ili kupata ngono, jambo linaloliachia familia njaa na kukosa fedha za kujikimu, huku wasichana wakiathirika zaidi.

Kwa mujibu wa maelezo ya kinamama ambao wanaume wao ni watuhumiwa, wanadai baada ya kuuza mazao wanaziacha familia bila chakula ndani na kusababisha watoto pamoja na wanafunzi wa kike kukosa mahitaji na kutumbukia kwenye vishawishi vinavyovuruga maisha yao.

Hali hiyo imeibua sauti ya mwanafunzi wa Shule ya Msingi Igegu (jina tunalolihifadhi) mwenye miaka 14 anayeeleza kukatishwa masomo akipewa ujauzito na kaka ambaye ni ndugu wa ukoo, anayemtaja kwa jina la Doto Ngassa (22).

“Nalelewa na mjomba wangu ambaye muda wote yuko na shughuli za shambani na pale ninapoomba mahitaji ya shule hususani sabuni, daftari, kalamu na pesi nakosa na kulazimika kuomba kwa kaka aliyekuwa anafanyakazi na kampuni ya raia wa China.”

Anadai alikuwa anampatia Sh.2,000 na wakati mwingine 5,000 alizozitumia kununua mahitaji ya shuleni hasa kalamu, daftari, mafuta ya kupaka na sabuni za kuoga na kufua.

Anasema, mahitaji hayo yalilazimisha kunyanyaswa kingono na anakutana na kaka yake siku za mkesha wa harusi kijijini kwao zinazofanyika usiku.

Anasema licha ya kwamba alikuwa anamfanyia vitendo vya ukatili hakutoa taarifa popote na hata alipopata ujauzito hakujua hadi alipogunduliwa na walimu waliompeleka hospitali kupimwa.

“Mimi nilikuwa na ndoto ya kuwa mwalimu, nimeishia njiani baada ya kupata ujauzito wakati nikijitafutia mahitaji ya shule niliyoyakosa kwa mjomba wangu. Nina ndoto ya kujifunza cherehani nipate fedha za kujikimu na mtoto wangu,” anasema.

Msichana huyu ni mfano wa mamia ambao wanakutana na tatizo na anashauri utafiti ufanyike na kupatikana ufumbuzi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Igegu anakosoma msichana huyo, Leme Solo, anasema, mwanafunzi huyo alikuwa anafanya vema darasani hasa walipokuwa wakiwapima kwenye mitihani mbalimbali na walipoona anabadilika walimpeleka zahanati na kubainika ni mjamzito.

Anasema, walimsimamisha masomo hadi atakapojifungua na polisi wanaendelea kumtafuta mhusika kwa hatua za kisheria na tukio hili ni la pili kutokea shuleni hapo.

Aidha, anaeleza kuwa matatizo ya mabinti shuleni ni mengi na baadhi ya wanafunzi wa kike wamekuwa wakirubuniwa kufanya vibaya kwenye mitihani yao ya mwisho ili wasifaulu na kuendelea na masomo na wengi wanakubali na kuandika matusi. Baada ya kufeli ndani ya miezi miwili wanapata taarifa za kuozeshwa huku wazazi na walezi kupewa ng’ombe, anasema.

Akizungumzia juhudi za kupunguza tatizo anasema mabaraza ya watoto shuleni yamelipunguza kwani baadhi yao wamekuwa wakitoa taarifa na kuwashauri nini cha kufanya, kuwafuata wazazi na walezi ili kuwashauri, kuwaelimisha umuhimu wa elimu anasema Solo.

Kadhalika, anaongeza kuwa wanafunzi wa kiume wanatoroshwa na kuwapeleka Rukwa na Tabora kufanyakazi mashambani na kuchunga mifugo hasa ng’ombe ili kupata ujira wa kuendesha familia wanazotoka.

“Kinachotumika kuwarubuni ni madai ya hata waliohitimu vyuo vikuu hawana kazi.” Anasema Solo.

“Wanafunzi wanaotoroshwa wanaotoka katika mazingira magumu, na wengi unapowafuatilia unakuta wanalelewa na mzazi mmoja au ndugu zao, hivyo wanakosa msukumo wa kuendelea na masomo na mwisho wanatekwa na kutokomea kwenye hisia za kutafuta maisha,” anaongeza.

Mwalimu wa malezi Sekondari ya Kaselya, Theodora Mdagachule anasema, wamebaini wanafunzi wengi wa kike wanakatisha masomo kwa kupata ujauzito baada ya kujiingiza kwenye vishawishi vya mapenzi wakati wakitafuta mahitaji muhimu ya shule pamoja na taulo za kike wanazozikosa kwa wazazi au walezi wao.

Theodora anasema, wametenga moja ya chumba cha vyoo vya wanafunzi wa kike kuwa chumba maalumu kwa kubadilishia taulo za kike ili kuwapa wasichana faragha na sasa mahudhulio ya wanafunzi yameongezeka kulinganisha na ilivyokuwa hapo awali na pia wanawapatia pedi.



Mwandishi Shaban Njia, akizungumza na mwanafunzi aliyekatisha masomo baada ya ujauzito. **PICHA: MWANDISHI WETU**

**MAKAHABA MASHAMBANI**

Mkazi wa Kijiji cha Mwamala B Salima Sosoma, anasema, wasichana wanakosa mahitaji muhimu akiwatuhumu wanaume kuwahonga ‘dada poa’ magunia ya mpunga ili wapate ngono badala ya kuuza kupata fedha za kuhudumia familia na kutunza akiba ya chakula.

Anasema, vijijini kumejaa wanawake warembo kutoka mjini wanaojificha katika mwamvuli wa biashara ya vinywaji lakini wakiuza miili yao kwa ujira wa kubadilisha debe moja la mpunga hadi gunia zima na kuwaingiza vijana kwa wazee kwenye biashara ya ngono na kusababisha familia kukosa chakula na mahitaji.

“Ikumbukwe wanawake wa Kisukuma hatuna sauti mbele za wanaume zetu na ukijifanya mjuaji unaadhibiwa mbele ya watoto hivyo haya yanayojitokeza tunaomba serikali iingilie kati na kuondoa wanaojihusisha na biashara za ngono kwa kutapeli mazao yao vijijini,” anasema Salima.

Ester Kenedy, ni mzazi anayesema nyakati za usiku wanawake hao wamejaa kila mahali wakijificha kwenye kuuza vinywaji katika ‘grosari’, baa na mitaani huko vijijini na kutaka hatua zichukuliwe kudhibiti.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Mwamala, Suzana Kayenge, anasema, wanajipanga kuanzisha msako wa wanaoshiriki kwenye utapeli wa mazao kwa ngono na kwamba watashirikia na Kamati za MTAKUWWA na serikali za vijiji kufanikisha azma hiyo.

Anaeleza kuwa wameweka utaratibu wa kupima maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa vijana wanaotaka kuolewa na kuoa kwa lengo la kukabiliana na maambukizi hayo yasiendelee kusambaa kwenye jamii.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata Sophia Filbert anasema, wameendelea kuwafikia wanafunzi shuleni, wazazi na walezi kuwapatia elimu ya ukatili wa kijinsia kwa kubainisha adhabu na madhara yake na pia kwa vijana na kinababa wanaongoza kwa kuuza vyakula kwa kubadilishana mpunga kwa ngono.

ELIMU

NA BEATRICE PHILEMON

# Baada ya kuchelea kudaka fursa EAC, vijana sasa wasukwa kuzichangamkia



Peterson Godfrey, mwanafunzi wa mwaka wa tatu IAA, akielezea umuhimu wa vijana kuwa sehemu ya EAC kiuchumi. **PICHA: FUNGUA TRUST**

ONGEZEKO la ushirikiano na uwekezaji kiuchumi ndani ya mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), wenye wanachama nane, linawaibua wadau wa elimu kuwafunza wana vyuo vikuu vya Tanzania, kuzitambua na kuzichangamkia fursa zinazopatikana.

Programu ya kutambua na kunufaika na fursa hizo, hivi karibuni imeanza na kuwafunza wanafunzi 300 wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) mbinu za kuchangamkia fursa za maendeleo zilizopo ndani ya EAC.

Taasisi ya The Fungua Trust, inayowanoa na kuwaingiza wasomi hao kwenye kuchachalika na kutambua fursa, inaeleza kuwa kumekuwa na ongezeko la masuala mengi yanayohitaji ushiriki wa vijana wa Tanzania.

Inataja biashara za hoteli, utalii, usafiri na usafirishaji wa watu na shehena, biashara za kilimo na nyingine mbalimbali za viwandani ambazo vijana Watanzania wanaweza kuzichangamkia.

Fatma Baraka maarufu. Bi Kidude.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa The Fungua Trust, Dk. Shogo Mlozi-Sedoyeka, anazungumza na Nipashe kuhusu mkakati huo, anasema ziko fursa za maendeleo zinazopatikana ndani ya EAC ambazo ni pamoja na wataalamu wa TEHAMA, uhandisi, usimamizi wa biashara na masoko.

EAC ina wanachama nane -Tanzania, Kenya, Uganda, Sudan Kusini, Congo -DRC, Burundi, Rwanda na Somalia.

Ndani ya jumuiya wanachama hutoa nafasi za masomo na mafunzo na pia kubadilishana uzoefu, anasema Dk. Shogo, ambaye ni Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki.

Anaongeza: Mafunzo yanayotolewa kwa wanafunzi wa IAA ni ili kuongeza uelewa kuhusu mtangamano hususani fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii zilizopo kama vile ajira na nafasi za masomo."

Fungua Trust imetoa mafunzo kama hayo kwa wasomi wa vyuo vikuu vya Dar es Salaam (UDSM) na Zanzibar (SUZA) mwaka jana, ili kuwapa uelewa wanafunzi anaeleza Dk. Shogo.

Akieleza sababu ya kuchukua hatua hiyo anasema ni baada ya kubaini kuwa ni wanafunzi au vijana wachache sana nchini wenye msukumo wa kuchangamkia fursa zilipo nje ya mipaka.

"Moja kati ya sababu za ufinyu wa ushiriki wa vijana ndani ya jumuiya ni ufahamu mdogo wa masuala ya mtangamano hasa muundo wa ushirikiano pamoja na hatua mbalimbali ambazo zinachukuliwa kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Kwa mantiki hiyo mafunzo haya yanalenga si tu kuongeza ufahamu wa masuala ya jumuiya, bali kuwajengea uwezo na stadi vijana ili kuwawezesha kufaidika na fursa zilizopo," anasema.

Akizungumza na wanafunzi, Spika wa Bunge la Afrika Mashariki, Joseph Ntakirutimana, anasema mafunzo yataleta mabadiliko, hamasa na maendeleo kwa vijana kuitumia jumuiya kwa tija zaidi.

Anaeleza kuwa vijana ndio nguzo kubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika kila nchi mwanachama na kwamba kutokana na umuhimu wao, Machi mwaka huu Bunge la Afrika Mashariki limepitisha azimio la kuanzishwa tawi maalum la vijana kuangalia masuala yao kwa ukaribu.

Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha, Profesa Eliamani Sedoyeka, anasema ushirikishwaji huu ni muhimu hasa kutokana na ukaribu kijiografia uliopo kati ya IAA na makao makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwataka wanachuo kuziona fursa.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO) Tanzania anayesimamia nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi, Caroline Khamati Mugalla, anaeleza kuwa masuala ya vijana yana nafasi kubwa katika shughuli na miradi mbalimbali ya shirika hilo.

"Vijana ndio nguvu kazi inayotegemewa kuleta maendeleo katika kila nchi mwanachama wa ILO, cha muhimu kuhusu nguvu kazi hii si idadi yao pekee bali ubora."

Anasema ILO inatekeleza miradi kadhaa kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau mbalimbali ndani ya EAC inayolenga kujenga uwezo wa vijana kujiari au kuajiriwa.

Moja kati ya miradi hiyo ambayo Chuo cha Uhasibu Arusha ni mnufaika, ni uendeshaji wa mafunzo ya shahada kwa njia ya uanagenzi, yanayompa mwanafunzi muda wa kutosha kujifunza akiwa katika maeneo ya kazi hivyo kuwaimarisha stadi zao za kazi kwa haraka.

Kutokana na uzoefu wake katika ushiriki na uendeshaji wa miradi ya taaluma, tafiti, na ubunifu ndani ya jumuiya, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) inatoa mada kwenye mafunzo hayo.

Dk. Judith Leo, akizungumza anasema NM-AIST ina programu mbalimbali za mafunzo na kujenda uwezo kwa vijana, pamoja na maeneo mengine taasisi hiyo inajengea vijana stadi za uandaaji wa maandiko ya miradi, na uanzishaji na ukuzaji wa miradi ya biashara.

Pia taasisi hiyo inatoa udhamini wa masomo na kutawatafutia wanafunzi nafasi za mafunzo ya vitendo ndani na nje ya nchi.

Katika mada yake elekezi, mwezeshaji wa mafunzo Profesa John Ruhangisa, kutoka Chuo Kikuu cha Makumira, aliyewahi kufanyakazi Jumuiya ya Afrika Mashariki, anasisitiza kwa washiriki umuhimu wa kufanya mabadiliko ya haraka ya fikra.

Pamoja na juhudi za jumuiya kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii kutokana na kukua kwa kasi kwa uchumi bado fursa hizi zina ushindani mkubwa mbali na ufaulu mzuri wa masomo katika fani za kitaaluma, ni muhimu kwa mwanafunzi kuwa na stadi na ufanisi katika maeneo mengine.

Akitoa mifano hai, Profesa Ruhangisa, anasema pamoja na mambo mengine, mwanafunzi ni lazima ajue jinsi ya kuandaa wasifu binafsi unaokidhi soko la ushindani, awe na umahiri wa uwasilishaji wa wazo au mradi, kujieleza na mawasiliano kwa ujumla.

Mbali na hilo, aliwaeleza wanafunzi hao kuwa ingawa mitandao ya kijamii na tovuti vimerahisisha sana upatikanaji wa taarifa, bado vijana wengi hawaitumii kwa manufaa yao.

"Ni vyema wanafunzi wakajua kuwa yale ambayo hawayasomi katika fani za kitaaluma wanaweza kuyapata kupitia mitandao hii," anasema.





# Polisi: Maofisa watendaji msigeuke mahakimu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Theopista Mallya, amewataka maofisa watendaji wa kata, vijiji na wenyeviti wa serikali za mitaa na vitongoji kuacha kujigeuza mahakimu kwa kutoa hukumu kwa kesi za jinai na kusababisha vitendo vya uhalifu kukithiri jijini hapa.

Aidha, Kamanda huyo amewataka viongozi hao kutojihusisha na vitendo vya kuwaficha wahalifu kwenye maeneo yao badala yake wasimamie sheria kwa kuwapeleka mahakamani.

Mallya, alisema hayo jana wakati akizungumza na wenyeviti wa serikali za mitaa wa Jiji la Dodoma kwenye kikao cha kujadili hali ya ulinzi na usalama wa mali na wananchi.

Alisema baadhi ya watendaji na wenyeviti kwenye maeneo yao wamekuwa wakijifanya mahakimu wa kuamua kesi za jinai badala ya kuzipeleka mahakamani.

Mallya, alisema kwa sasa hali siyo nzuri jijini hapa kutokana na kujitokeza kwa vitendo vya uhalifu vya uvunjaji nyumba usiku na mchana, uporaji kwa kutumia bodaboda, utapeli kwa njia ya mitandao ya simu na wizi wa mifugo.

Aliutaja uhalifu mwingine ambao umekuwa ukihatarisha uvunjifu wa amani ni pamoja na baadhi ya watendaji na wenyeviti wao wa serikali za mitaa, vitongoji kujiingiza kwenye biashara za kuuza ardhi kwa wawekezaji na kusababisha migogoro.

Kwa mujibu wa Mallya, kutokana na taarifa hizo amewataka wasimamizi hao wa ngazi ya kata, vijiji, mitaa na vitongoji kusimama kwenye nafasi zao kama walivyoapa kwa kutenda haki kwa maamuzi pale wanapowajibika kuwatumikia wananchi wao.

Alisema wao kama wasimamizi wa ulinzi na usalama kwenye maeneo yao wanatakiwa kutowafumbia macho wahalifu wanaokamatwa kwa hofu ya kuharibu mahusiano na wazazi na walezi wanaoishi nao.

Alisema kuna vitendo vingi vinafanyika ikiwamo ubakaji wa watoto wa kike na ulawiti, lakini baadhi ya watendaji wamekuwa wakimaliza kesi hizo kienyeji.

# Biteko asifu wanafunzi, shule bora kutotangazwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, amesema uamuzi wa Wizara ya Elimu kuacha kutangaza shule 10 bora katika mitihani ya taifa umesaidia kuondoa ubaguzi kwa wanafunzi.

Biteko alisema hayo juzi jijini hapa kwenye mkutano wa walimu wa shule mbalimbali za jiji la Dodoma.

Alisema kitendo kilichofanywa na wizara hiyo kuondoa utaratibu wa kutangaza wanafunzi bora na shule kumesaidia kuondoa ubaguzi.

Alisema walimu wanapaswa kutengeneza taifa kwa kuhakikisha wanazalisha kizazi ambacho kitakuwa na manufaa makubwa kwa nchi na kuwatenganisha.

"Hakikisheni mnazalisha wanafunzi waliobora msitumie kigezo cha akili kuwagawa wanafunzi mkifanya hivyo mtakuwa mnazalisha taifa lisilo bora," alisema Biteko na kusisitiza kuwa:

"Walimu mnayo kazi kubwa ya kututengenea Taifa kwa kutafsiri R4 za Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan hasa kwenye suala la maridhiano."

Kwa upande mwingine, aliwataka walimu kuwafundisha kwa umakini wanafunzi ili wazidi kufanya vizuri na kutafsiri kwa vitendo maono ya Rais Samia na Mbunge Dodoma, Anthony Mavunde katika kuhakikisha elimu bora inatolewa.

Dk. Biteko alisema mataifa yaliyoendelea uwekezaji wake upo katika elimu na ndiko alikowekeza Rais Samia.

Kwa upande wake, Mavunde ambaye ni Waziri wa Madini, alisema lengo la mkutano huo ni kujadili changamoto katika sekta ya elimu katika muhula uliopita na wafanye nini katika muhula ujao ili kuendelea kuwatia moyo walimu.

"Tuliona njia pekee ya kufanya vizuri ni kuwaweka walimu pamoja hatutaki mwalimu wetu akiwa na changamoto akalalamike kwani haya ni sehemu ya maisha yetu," alisema Mavunde.

Alisema kupitia mkutano huo watazungumza na kuweka utaratibu mzuri wa kutatua kero.

"Dhamira yangu ni ya dhati katika kukuza elimu kwani nimeweza kujenga shule za msingi na sekondari kwa wanafunzi waliokuwa wakitembea umbali mrefu," alisema Waziri Mavunde.

Alisema kwa kushirikiana na baadhi ya wadau wameweza kujenga uzio katika shule mbalimbali kusaidia watoto kusoma kwa utulivu.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, alisema Mavunde anathamini elimu na kila anapokutana naye huwa anahoji kuhusu miradi ya sekta hiyo katika jimbo lake.




Baadhi ya wanafunzi wa Shahada ya awali ya Uandishi wa Habari na Mahusiano ya Umma (BAJP), kutoka katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakifurahia kutimiza ndoto yao ya kuchapisha gazeti la kujifunzia lililochapishwa na Kampuni ya The Guardian hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanakijiji watatuliwa kero kusotea maji

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IRAMBA

ZAIDI ya wakazi 4,192 wa Kijiji cha Migilango wilayani hapa Mkoa wa Singida wanatarajia kuondokana na kero ya ukosefu wa majisafi na salama kufuatia kukamilika kwa mradi wa maji.

Mradi huo uliogharimu Sh.246,914,000 umejengwa kwa ufadhili wa Poul Due Jensen Grundfos Foundation ya nchini Denmark kupitia asasi isiyo ya kiserikali ya Water Gate Community Link ya Dar es Salaam kwa ushirikiano wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Iramba, Mhandisi Ezra Mwacha, akizungumza juzi wakati wa uzinduzi na kukabidhi mradi huo kwa mkandarasi wa Kampuni ya BC Water Equipment Limited, alisema utawezesha jamii kupunguza unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake, watoto na wanafunzi ambao walikuwa wahanga wakubwa wa kutafuta maji.

Mwacha, alisema manufaa mengine ya mradi huo ni kuwawezesha wananchi kuepuka maradhi yaliyokuwa yakisababishwa na ukosefu wa majisafi na salama na kutembea umbali wa kilometa 14 kufuata huduma hiyo.

Mtendaji Mkuu wa Water Gate Community Link, John Mudende, alisema mradi huo utakuwa na ujazo wa lita 50,000 na kutakuwa na vituo vinne vya kuchotea maji wananchi wa kijiji hicho.

Alizitaka mamlaka za maji za wilaya na wananchi kuhakikisha wanatunza miundombinu ya mradi huo isiharibiwe.

"Mradi huu umejengwa kwa fedha za wananchi wa huko duniani ambao walipambana na kuweka akiba ili sisi wananchi wa Tanzania hususani wa kijiji hiki cha Migilango waweze kupata maji na hivyo kwenda na sera ya serikali ya kumtua ndoo mama kichwani," alisema.

Meneja wa Tanzania wa Groundfos Foundation, Ngusa Breck, alisema fedha ambazo zitakuwa zinakusanywa wakati wa kuuza maji zitunze kwa ajili ya kugharamia matengenezo ya miundombinu itakapokuwa na changamoto.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, akizungumza baada ya kuzindua mradi huo, aliwashukuru wafadhili kwa kuongeza kiwango cha upatikanaji maji vijijini kufikia asilimia 68.





# Kibano chaja watakaokaidi kulipa kodi ya ardhi

**Na Munir Shemweta**

NAIBU Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, amewahimiza wamiliki wa ardhi nchini kuhakikisha wanalipa kodi kwa wakati ili kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pinda alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa kuhusiana na zoezi la ukusanyaji kodi ya pango la ardhi baada ya Waziri wa Ardhi, Jerry Silaa kuwapa wamiliki wanaodaiwa kodi hiyo kuhakikisha wamelipa kufikia Juni 10, mwaka huu.

"Naomba kusisitiza kwa wamiliki wote wa ardhi nchini, kutekeleza sharti la kulipa kodi ya ardhi kwa kuwa sasa tumeboresha njia za ukadiriaji na ulipaji wa kodi husika kidigitali," alisema.

Aliwakumbusha wamiliki wa ardhi maelekezo yaliyotolewa na Silaa wakati wa kuhitimisha hotuba ya bajeti ya mwaka huu Bungeni kwamba wizara hiyo imedhamiria kuchukua hatua kwa wamiliki wote wa ardhi watakaoshindwa kutimizi masharti ikiwamo kufikishwa mahakamani ili kuuza mali zao kufidia kodi ya ardhi na kupendekeza ubatilisho wa milki zao.

Pinda, alisema wamiliki wa ardhi wanaweza kupokea ankara za malipo kupitia ofisi za ardhi za mikoa na halmashauri baada ya kupata makadirio ya kodi wanayodaiwa na kulipa kupitia benki au kwa wawakala wa taasisi hizo za fedha.

Alisema vilevile wanaweza kulipa kwa njia ya simu ya kiganjani kwa kufuata taratibu za miamala ya malipo ya serikali.

Naibu Waziri huyo alifafanua kuwa malipo ya kodi ya pango la ardhi hufanyika kwa kuzingatia ukubwa wa ardhi inayomilikishwa, matumizi ya ardhi yaliyoidhinishwa, thamani ya ardhi na kiwango cha malipo ya mbele ya ardhi inayomilikishwa.

Aliwataka wamiliki wa ardhi waliopimiwa kuhakikisha wanakwenda ofisi za ardhi kumilikishwa kwa kuwa wasipofanya hivyo baada ya siku 90 wataingizwa kwenye mfumo na kuanza kudaiwa kama wamiliki wengine.

Akizungumzia kuhusu mkanganyiko uliopo baina ya kodi ya pango la ardhi na kodi ya majengo, alisema ya pango la ardhi hutozwa kwa wamiliki wa ardhi.

Alisema kwa upande wa kodi ya majengo hutozwa kwenye kuwekewa utaratibu wa ulipaji na ukusanyaji wake.

Alisema kwa sasa inalipwa kwa njia ya malipo ya ununuaji wa umeme kupitia mfumo wa LUKU.

Hivi karibuni Waziri Silaa aliwapa wamiliki wa ardhi zikiwamo taasisi za umma zinazodaiwa kodi ya pango la ardhi kuhakikisha wamelipa hadi kufikia Juni 10, mwaka huu, lasivyo, hatua za kisheria zitachukuliwa kwa watakaokaidi amri hiyo.



Baadhi ya wajasiriamali wa eneo la Kabwe jijini Mbeya, wakiendelea kuuza viatu pembezoni mwa barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) baada ya kuondolewa katika eneo la Stendi ya Kabwe kutokana na kuuza bidhaa zao nje ya maduka ya wafanyabiashara wengine na kusababisha migogoro. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# TCRA yazitega kampuni za simu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MAMLAKA ya Mawasiliano nchini (TCRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini imetishia kuzichukulia hatua kampuni za simu kwa kushindwa kudhibiti wafanyabiashara wa vocha kwa bei za juu.

Meneja wa TCRA wa Kanda hiyo, Bonface Shoo, alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kupanda kwa bei ya vocha katika baadhi ya maeneo.

Shoo, alisema ofisi yake imepokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wakazi wa mikoa ya Mbeya na Songwe wakidai vocha zenye thamani ya Sh. 500 wanauziwa kati ya Sh. 600 na 700 huku ile ya Sh. 1,000 kwa Sh. 1,200.

Alisema baada ya kupokea malalamiko hayo aliwaita watoa huduma wa mawasiliano na kuwahoji endapo wamefanya mabadiliko ya bei na kuthibitishiwa hawajafanya hivyo bali ni baadhi ya wafanyabiashara waliamua wenyewe.

Shoo, alisema aliwaagiza kufuatilia na kuwadhibiti wafanyabiashara hao kabla hatua za kisheria hazijaanza kuchukuliwa dhidi yao,

huku akiwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa kuhusu wale wote watakaohusika.

"Watoa huduma hawa ndio wenye wajibu wa kuwadhibiti wafanyabiashara, wakishindwa sisi tutawashughulikia wao, pia tunaviomba vyombo vya dola vitusaidie kuwadhibiti vijana hawa ambao wanakiuka sheria," alisema Shoo.

Alizitaka kampuni hizo kuchukua hatua dhidi ya wafanyabiashara hao wasiokuwa waaminifu, zitoe taarifa mapema kwa mamlaka hiyo ili kuwekwa kumbukumbu vizuri.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya, walisema kitendo cha wafanyabiashara kupandisha bei za vocha hizo kinyemela kinawaumiza kutokana na kuongeza ugumu wa maisha.

Zawadi Mwankina, alisema yeye ni mjasiriamali wa nguo na viatu kwa njia ya mtandao, anahitaji kuwa na muda wa maongezi na intaneti, kitendo cha vocha kupanda bei, kimeaathiri biashara zake.

Alisema wakati mwingine anahitaji kununua vocha ya Sh. 1,000, anapokuta bei ni Sh. 1,200 anashindwa, hivyo kulazimika kuwatembelea wateja wake kwa mguu.

Thobias Ole Kuja, alisema hawajawahi kusikia matangazo ya aina yoyote kuhusu mabadiliko ya bei za vocha na kwamba kitendo cha kuwashtukiza kiliwakera.

Ni zaidi ya mwezi mmoja sasa tangu liibuke tatizo la baadhi ya wafanyabiashara wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuuza vocha kwa bei ya juu tofauti na elekezi.

# Watendaji waagizwa kuhamasisha lishe bora kwa jamii

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Mbeya imewaagiza watendaji wa kata na vijiji kushirikiana na viongozi na wadau kuhamasisha lishe bora kwa watoto katika maeneo yao ili kukabiliana na utapiamlo.

Baadhi ya viongozi hao wanadaiwa kuwa wamekuwa wakiwaachia maofisa lishe pekee kufanya kazi hiyo hali ambayo inapunguza ufanisi na kusababisha tatizo la udumavu kuendelea kukithiri kwenye maeneo yao kutokana na utapiamlo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbarak Batenga, alitoa agizo hilo wakati akiongoza kikao cha lishe cha robo ya tatu ya mwaka 2023/2024 kilichofanyika wilayani hapa.

Batenga alisema watendaji hao wakishiriki ipasavyo katika suala la lishe bora kwa familia zao itasaidia jamii ya sasa na baadaye kuwa na ustawi wa afya bora.

Aliwataka viongozi hao kushirikiana na wahudumu wa afya ngazi za kata na vijiji kusimamia lishe ili kuhakikisha jamii inatambua na kuzingatia umuhimu wake kama mikataba inavyoelekeza.

"Ni kweli tunao watendaji wa afya hasa maofisa lishe ambao wanalo jukumu la kusimamia masuala ya lishe katika maeneo yetu, lakini pekee yao hawataweza, hivyo ili jambo hili lifanikiwe kwa ufanisi kila mtendaji anapaswa kushiriki ipasavyo kwenye shughuli za lishe," alisema Batenga.

Mganga Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Darison Andrew, aliwahimiza wanajamii kuzingatia ushauri wa kitaalamu juu ya kuzingatia lishe bora kwani athari za kukosekana kwake ni vigumu kurudi katika hali ya kawaida ndani ya jamii.

Alisema ukosefu wa lishe bora huathiri mfumo wa kufikiri hivyo ikiwa jamii itawekeza kwenye lishe itasaidia kuwa na kizazi sahihi na chenye uwezo mzuri wa kufikiri pamoja kuondokana na udumavu.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Rehema Hiluka, aliwaomba viongozi na wananchi kushirikiana kuhakikisha lishe inazingatiwa katika maeneo yao ili kutokomeza udumavu.

Aliwaomba pia viongozi wa dini na mila kushiriki kwenye uhamasishaji ili kuhakikisha elimu hiyo inawafikia wananchi kwa wakati.



# Jaji afunda jamii usafi wa mazingira

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

JAJI Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Joachim Tiganga amesema jamii inapaswa kuogopa suala la usafi na uhifadhi wa mazingira kama sheria ya udhibiti wa nyara za serikali.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa Wiki ya Mazingira jijini Arusha alisema kuwa ametoa kauli hiyo kutokana na takwimu kuonyesha kwa sasa, tani milioni saba za taka ngumu zinazalishwa mjini, kati ya hizo asilimia 35 hukusanywa na kuteketezwa kwa utaratibu sahihi na salama.

Jaji Tiganga ambaye alimwakilisha Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma kwenye maadhimisho hayo ambayo kilele chake kinatarajiwa kufanyika kesho alisema kuwa:

"Kiasi kikubwa huzalishwa katika halmashauri za miji midogo, manispaa na majiji, huku takwimu zikionyesha kuwa ni asilimia 35 tu hukusanywa na kuteketezwa kwa utaratibu ambao ni sahihi na salama."

Awali Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, aliwataka wakazi wa Jiji la Arusha kuboresha usafi wa mazingira kuelekea msimu wa kupokea watalii unaonza mwezi huu.

"Hatuwezi kuwa na wageni katika Jiji ambalo wamachinga (wafanyabiashara wadogo) wanapanga bidhaa zao ovyo. Ni lazima tujipange na kuhakikisha jiji letu linavutia na hata mgeni akifika kwetu, atamani kurudi tena.

...siyo mgeni anafika anakuta mmepanga bidhaa tena vyakula kuanzia Philips mpaka Sanawari, halafu mnasema ni jiji la kitalii."

Mkurugenzi wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Hali ya Mazingira Ofisi ya Makamu wa Rais, Sigxibert Kavishe, alisema kwa Tanzania, suala la usafi lipo katika hatua nzuri na kulitaja Jiji la Arusha ni miongoni mwa maeneo yanayovutia kwa usafi.

"Tanzania tupo vizuri lakini pia hata hapa Arusha tunaona vile mazingira yalivyo na tunaendelea kuhamasisha wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kuwa mazingira yanapotunzwa huvutia na kuleta hewa safi," alisema.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Kaskazini, Benjamin Doto, alisema kauli mbiu ya mwaka huu ya maadhimisho hayo ni 'kurejeleza ardhi, kustahimili hali ya ukame na jangwa.'

Doto, alisema kadri binadamu wanavyoharibu mazingira, ndivyo wanavyojiweka katika hali ngumu ya kuweza kustahimili namna dunia inavyokwenda.

Alisema maelekezo waliyopewa na Jaji Mkuu ni kuwa utunzaji wa mazingira na usafi ni suala endelevu.

# Gwajima awakabidhi mabinti kompyuta

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amekabidhi kompyuta mpakato kwa mabinti 50 wenye umri wa miaka 18 hadi 25, baada ya kushiriki kambi ya kidijitali kwa ajili ya kuwasaidia kubuni miradi.

Kambi hiyo iliandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN Women), kwa ushirikiano na Tanzania Data Lab, ikiwa ni mpango wa miaka minne wa 'African Girls Can Code Initiative' (AGCCI), unaojulikana 'Binti Dijitali', unaofadhiliwa na serikali ya Ubelgiji.

Akikabidhi kompyuta hizo jana, jijini Dar es Salaam, Dk. Gwajima alisema kuwa ni dhamira ya serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, kuhakikisha wanawake na wasichana wanapata ujuzi wa kidigitali unaohitajika ili kuendelea kuwa na ushindani katika soko la kisasa.

"Hakuna swali, tunahitaji wasichana na wanawake zaidi katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM). Hii itahakikisha kuwa na usawa na fursa zinazozingatia haki za binadamu.

"Tukiweza kufanya hivyo sayansi na ujuzi, utafiti, ubunifu kwa wanawake utachangia kuwa na kundi hili kwenye ngazi za maamuzi, kuongeza usawa. Tanzania imejizatiti kuwajenga wasichana," alisema Dk. Gwajima.

Alisema kundi hilo lina haki ya kuifikia dunia ya kidijitali kwa kuwa ujuzi wao na ubunifu tunachangia kubadili maisha kijamii na kuwa sauti katika kupambana na ukatili wa kijinsia.

Mwakilishi Mkazi wa UN Women nchini, Peterson Magoola, alisema kuna haja ya kuongeza uwekezaji kwenye sayansi na teknolojia hususan kwa wasichana na wanawake.

"Kama wasichana na wanawake, wanaotakiwa kuwamo kwenye soko la ajira, wanahitaji elimu ya TEHAMA, hii itasaidia kuwa na watoa maamuzi kwenye sekta mbalimbali," alisema Magoola.

Mkuu wa Kitengo cha Ushirikiano kutoka Ubalozi wa Ubelgiji nchini, Fanny Heylen, alisema programu hizo zinalenga kuongeza idadi ya wasichana na wanawake kwenye majukwaa ya kidijitali ili kuwajumuisha katika ajira kwenye STEM.

Kupitia mradi huo, kompyuta 50 zitatolewa kwa mabinti wa visiwani Zanzibar wiki hii kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar.

Kadhalika, awamu mpya ya mradi wa AGCCI itazinduliwa Nairobi nchini Kenya Juni, mwaka huu.

Mpango wa AGCCI unalenga kupunguza mgawanyo wa kiteknolojia kwa kuongeza wanawake na wasichana upatikanaji wa teknolojia ya kisasa na kusaidia uwezeshaji wao kupitia elimu na ajira.

Duniani, wanawake na wasichana wako asilimia 25 katika dijitali huku nchini, ni mwanamke mmoja tu kati ya 10 ana kiwango fulani cha ujuzi wa kidijitali, kulingana na utafiti wa ITU wa 2020.

Ripoti ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ya mwaka 2019 inaonyesha ni asilimia 18 tu ya wataalamu walioajiriwa katika fani za sayansi na uhandisi ni wanawake.



Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah (kulia), akizungumza na mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Juma Ali Kharib ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha ADA-TADEA katika Baraza la Wawakilishi Chukwani nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SMZ yaanza kukabili uhaba madaktari wa wanyama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imeanza kulipatia ufumbuzi tatizo la uhaba wa madaktari bingwa katika fani ya wanyama baada ya kuajiri vijana 25 waliohitimu fani hiyo nchini China, imeelezwa.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk.Khalid Salum Mohamed kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Umwagiliaji wakati akijibu swali la mwakilishi wa viti maalum, Shadya Mohamed Suleiman katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, aliyetaka kujua hadi sasa serikali imechukua hatua gani kukabiliana na uhaba wa madaktari wa wanyama.

Dk. Khalid alisema katika miaka ya nyuma kulikuwa na tatizo kubwa la uhaba wa madaktari bingwa katika fani ya wanyama na mifugo kulikochangiwa na vijana wengi kutopenda kusomea fani hiyo.

Alizitaja sababu nyingine kuwa ni madaktari wengi waliosomea fani hiyo ikiwamo nchi za nje kustaafu utumishi wa lazima bila ya kuwapo kwa mbadala wa watumishi wengine.

Alisema hatua hiyo ililazimu serikali kusomesha vijana wengi zaidi nje ya nchi ikiwamo China, 23 wamehitimu masomo yao na kuanza kazi.

Alisema madaktari hao wamepelekwa Wilaya ya Unguja na Pemba ya kusaidia huduma za afya kwa wanyama ikiwa ni sehemu ya mikakati ya wizara kuimarisha mifugo katika uzalishaji wa nyama.

# Mwinyi kuzindua uwekezaji Bawe

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi anatarajiwa kuzindua mradi wa kwanza wa uwekezaji katika visiwa vidogo vilivyoko Kisiwa cha Bawe Juni 15, mwaka huu.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Khamis Suleiman Shibu wakati akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa.

Shibu, alisema baada ya mradi huo kuzinduliwa unatarajia utatoa zaidi ya ajira 400 kwa wananchi na unamilikiwa na wawekezaji kutoka nchini Italia na Luxembourg.

Alisema mwaka 2021, Serikali ya Zanzibar iliruhusu uwekezaji katika visiwa vidogo vilivyopo Unguja na Pemba, 17 kati ya 20 vilivyotangazwa katika awamu mbili tofauti, vimekodishwa kwa wawekezaji.

Shibu, alisema uwekezaji katika visiwa hivyo ni utekelezaji wa sera ya serikali ya kuimarisha uwekezaji kwenye sekta ya uchumi wa buluu.

Alisema uwekezaji huo utaongeza ukuaji kwenye pato la taifa kupitia kodi na mapato mengine yatakayokusanywa.

Alisema Sheria mpya ya Uwekezaji Zanzibar ya mwaka 2023 imeanza kutumika na kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji ikiwamo kutoa fursa na vivutio zaidi kwa wawekezaji.

Alisema sheria hiyo imeanzisha mamlaka ya kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), kikiwa ni chombo kinachosimamia utendaji kazi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NOEL ALEX KALILI**

anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye usajili namba **T 729 AXR**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/100320/2024**

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT**
**(Cap. 117 R.E. 2002)**
**CHANGE OF NAMES BY DEED POLL**

THIS DEED POLL is made this 26th day of September 2023
By THIS DEED POLL, I, the undersigned and the person with names PASCHAL POTI MINANGI a resident of Dar es salaam, a citizen of the united Republic of Tanzania by birth DO HEREBY ABSOLUTELY renounce and abandon the use of my former names of PASCHAL POTI NYANJA as variably used in National identity card so as to adopt the name of PASCHAL POTI MINANGI variably used in my voter's identification card and public service Social Security Fund identity card (PSSSF)
And in pursuance of such change name as aforesaid I hereby declare that I shall at all times hereafter in all records, deeds and instruments in writing and in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever related to my professional, use and sign the name of PASCHAL POTI MINANGI as my name in lieu of the said names of PASCHAL POTI NYANJA renounce as aforesaid.
THAT the reason for change is due to that, the name PASCHAL POTI MINANGI is the official name and used in my all documents.
AND I HEREBY AUTHORIZE and request all persons to designate and address me by such assumed name of PASCHAL POTI MINANGI only.
IN WITNESS WHEREOF I hereon substitute my old names of PASCHAL POTI NYANJA by the new name of PASCHAL POTI MINANGI

**SIGNED AND DELIVERY** at Dar es Salaam by the said **PASCHAL POTI MINANGI** introduced to me by ..........the latter known to me personally: on the 26th day of September 2023

DEPONENT



BEFORE ME
NAME: Bitwahiva
SIGNATURE: ______
ADDRESS: P.O.BOX 60548 DAR ES SALAAM

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RONALD MICHAEL KAJALE**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 240 DDZ.** Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN.102545/2024**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOSEPH RAJABU MAZENGO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. S4433-0008 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIDETE DAY SECONDARY SCHOOL mwaka 2015. Cheti cha kidato cha sita chenye index No. S0123-0753. kilichotolewa na Baraza la mitihani la taifa kupitia KWIRO SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. vyeti hivi vimepotea Korogwe Mjini – TANGA. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**Taarifa ya Polisi: PHQ/DOD/KON/21432/2024**
**Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/KON/21438/2024.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and administration Cause No 11794 of 2024**
**In the matter of the estate of the late**
**STEPHANO WILLIAMU SAUSI of Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by ELIZABETI STEVENI WILLIAMU**

**GENERAL CITATION**

**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 11 day of 6......................2024
Dated at Dodoma this 23 day of 5................2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

## ANATAFUTWA



BWANA **MAYUNGA MASAI** WA IFAKARA ANAMTAFUTA NDUGU YAKE (MWENYE PICHA HII) BWANA NGUSA MAFULAYA NGONGOLI, ALIYEPOTEZANA NAYE TANGU 2014 MARA YA MWISHO ALIKUA AKIISHI IFAKARA NA BAADAE ALIHAMIA DODOMA, ATAKAYEMUONA AU KUJUA TAARIFA ZAKE **TUPIGIE 0785987554/0652873452.**
**POLISI TAARIFA: POL/TZR/IFA/RB/14/2024**

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB NA:**
**CDA/ED/LA-15/62321 MMILIKI ALIYEANDIKISHWA:**
**HASSAN MAKATA MAKERO**
**ARDHI: KIWANJA NA. 55 KITALU 'F' ENEO LA MIGANGA WEST**
**MUOMBAJI: FEDISTER AGREY MELELE**

**TAARIFA IMETOLEWA,** kwamba Barua ya Toleo iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa hati Milki mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti la serikali/ magazeti ya kawaida yaliyopo kwenye jamii.
BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI ikionekana, irudishwe kwa **:**

**Mkurugenzi,**
**Halmashauri ya Jiji,**
**P. BOX 1249,**
**DODOMA**
**Imetolewa na:**
..................................
**Georgina Kallaghe**
**Afisa Ardhi Mteule**
**DODOMA,**
**09 Mei, 2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**USINGA ALLY HAJI**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba MC286 CPJ. Kwa yeyote atakaeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/SIN/SIN/3800/2024**

---

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

**JAMES REVELIAN KAHATANO**

anatangaza kupotea kwa kadi za bajaji zenye usajili namba MC 621 ACA, MC 748 BCF, MC 281 BLT, MC 685 CLY, MC 492 CSZ, M C 979 CYU, MC 648 DDS , MC 190 DVQ na MC 902 EAJ. Kwa yeyote atakaezeziona atoe taariifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/106430/2024**

---

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN ADAM SUMBIZI** anataangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 0583-0147 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kwa kupitia MAZINYUNGU SECONDARY SCHOOL mwaka 2010. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/5229/2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro**
**Mkoa Geita**
**Shauri la madai Na. 63/2022**
**Jina la Mdai kapaya s/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Lukia D/O Omary**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji mashauri mahakama za mwanzo)**

**KWA Lukia D/O Omary wa kilima hewa**
Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 4 Mwezi 6 Mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 mwezi wa 5 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro Mkoa Geita**
**Shauri la Madai Na 35 2021**
**Jina la Mdai Kapaya Dotto**
**Jina la mdaiwa Nkonoki janikila**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

KWA Nkonoki Janikila wan jia panda Katoro KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu Ya Shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ua Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 06 mwaka 2024 kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 Mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro**
**Mkoa Geita**
**Shauri la madai Na.136/2022**
**Jina la Mdai kapaya s/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Adamu s/o Shadrack**
**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji mashauri mahakama za mwanzo)**

**KWA Adamu s/o Shadrack wa Mtakuja - Katoro**
Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 4 Mwezi 6 Mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 mwezi wa 5 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro**
**Mkoa Geita**
**Shauri la madai Na.139/2022**
**Jina la Mdai kapaya s/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Joseph s/o Bunzari**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji mashauri mahakama za mwanzo)**

**KWA Joseph s/o Bunzari wa Kilimahewa Katoro**
Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 4 Mwezi 6 Mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 mwezi wa 5 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro**
**Mkoa Geita**
**Shauri la madai Na.134/2022**
**Jina la Mdai kapaya Dotto**
**Jina la mdaiwa Juma Mathias**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(kanuni ya 62 ya kanuni za uendeshaji mashauri mahakama za mwanzo)**

**KWA Juma Mathias wa Katoro Senta**
Kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwaajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 4 Mwezi 6 Mwaka 2024 kueleza kwanini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 29 mwezi wa 5 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro Mkoa Geita**
**Shauri la Madai Na 99 /2022**
**Jina la Mdai Kapaya S/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Marco S/o Mshindikwa**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA Marco S/o Mshindikwa wa Masolwa wa Ludete**
KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu Ya Shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ua Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 06 mwaka 2024 kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 Mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro Mkoa Geita**
**Shauri la Madai Na 140 /2022**
**Jina la Mdai Kapaya Dotto**
**Jina la mdaiwa Mateso Peter**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA Mateso Peter wa Bugaja Mbelele**
KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu Ya Shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ua Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 06 mwaka 2024 kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 Mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro**
**Mkoa Geita**
**Shauri la Madai Na 132 /2022**
**Jina la Mdai Kapaya S/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Retisia D/o Masolwa wa Katooro**
**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA Retisia D/o wa Masolwa wa Katoro**
KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu Ya Shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ua Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 06 mwaka 2024 kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 Mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO YA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Geita**
**Kituo cha Katoro Mkoa Geita**
**Shauri la Madai Na 63 /2022**
**Jina la Mdai Kapaya S/o Dotto**
**Jina la mdaiwa Mtita S/o Seif**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**
**(Kanuni ya 62 ya Kanuni za Uendeshaji mashauri Mahakama za Mwanzo)**

**KWA Mtita S/o Seif wa Kilima Hewa**
KWAMBA Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu Ya Shauri tajwa hapo juu unatakiwa kufika mbele ua Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 06 mwaka 2024 kueleza kwa nini Hukumu isitekelezwe dhidi yako. Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 28 Mwezi 05 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA)**
**DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA RUFAA YA MADAI NA. 2648/2024**
**MUTABAAZI JULIUS LUGAZIYA..................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KENNEDY @ KEN MGIMBA...............MJIBU MAOMBI NA. 1**
**DIANA KAGO....................MJIBU MAOMBI NA. 2**
**KWA:**

- **KENNEDY @ KEN MGIMBA**
- **DIANA KAGO**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji aliyetajwa hapo juu, amefungua shauri la maombi ya madai dhidi yako, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinapatikana katika mahakama hii kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii wewe mwenyewe au wakili au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe 25/06/ 2024 saa tatu kamili (3:00) asubuhi mbele ya Mhe. Jaji B.K Philip kujibu maombi hayo dhidi yako. Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia katika utetezi wako siku hiyo.
**ANGALIA**
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama leo tarehe 28/05/2024

28/05/2024

---

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# ANC kuanza kuunda serikali ya mseto

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

CHAMA tawala nchini Afrika Kusini 'African National Congress' (ANC), kimesema kitaanza mazungumzo na vyama vingine kuunda serikali mpya baada ya kupoteza wingi iliokuwa nao kwa miongo mitatu.

Ikiwa tayari asilimia 99.91 ya kura zikiwa zimehesabiwa baada ya uchaguzi wa Jumatano, Chama cha Rais Cyril Ramaphosa cha ANC kilikuwa kimepata asilimia 40.2, matokeo ambayo ni mabaya kulinganisha na mwaka 2019 ambako kilishinda asilimia 57.5 ya kura.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Katibu Mkuu wa chama hicho, Fikile Mbalula, alisema ANC kimejitolea kuunda serikali itakayodhihirisha ari ya umma, iliyo imara na inayoweza kuongoza vizuri.

Inaelezwa kuwa Chama cha ANC kinalazimika kuunda serikali ya mseto na kuwashawishi wengine waunge mkono kuchaguliwa tena kwa Rais Ramaphosa bungeni ili kumruhusu aunde serikali ya wachache.

Mbalula alisema chama hicho kitafanya mazungumzo ya ndani na pia makundi mengine katika siku chache zijazo katika hatua za kutafuta uungwaji mkono.

Pia matokeo hayo yanaashiria mageuzi makubwa kwa Afrika Kusini kwa kuwa chama hicho kimefurahia wingi bungeni tangu 1994, wakati shujaa wa ukombozi Nelson Mandela alipoiongoza nchi hiyo kutoka kwa utawala wa wazungu wachache na kuielekeza katika demokrasia.

"Matokeo haya yanatuma ujumbe wa wazi kwa Chama cha ANC, Tungependa kuwahakikishia watu wa Afrika Kusini kwamba tumewasikia. Tumesikia wasiwasi wao, kufadhaika kwao na kutoridhika kwao," alisema Mbalula.

Katika hatua nyingine, baadhi ya vyama vya siasa vimedai kuna mapungufu katika uhesabuji na ujumuishaji wa kura. Chama kikubwa na chenye ushawishi cha rais wa zamani Jacob Zuma, uMkhono weSizwe (MK) kiliwaonya maofisa wa tume ya uchaguzi dhidi ya kusonga mbele na mchakato wa kuyatangaza matokeo ya mwisho.

"Kama hilo litatokea, mtakuwa mnatuchokoza," Zuma, mwenye umri wa miaka 82, alisema, akilalamika kuhusu masuala nyeti ambayo hakuyaeleza wala kuwasilisha ushahidi wa kuunga mkono madai yake. Data kutoka kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya Afrika Kusini, (IEC), zimeonyesha chama cha MK kiko katika nafasi ya tatu na asilimia 14.59 ya kura, matokeo ya kushangaza kwa chama kilichoundwa miezi michache tu iliyopita kama chombo cha kumwezesha rais wa zamani wa ANC Jacob Zuma kugombea katika uchaguzi.

Lakini wakati wote wa kampeni chama cha MK kiliwaambia wafuasi wake kingeshinda theluthi mbili ya kura. Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi Mosotho Moepya alisema tume hiyo itafuatilia na kuchunguza kila madai yaliyowasilishwa mbele yao na ilikuwa imeamuru kura zihesabiwe upya katika matukio 24.

Chama cha ANC sasa kitalazimika kugeukia wapinzani kutoka upande wa kushoto au kulia kuunda serikali. Chama kinachofuata siasa za wastani za mrengo wa kulia cha Democratic Alliance, DA, kilishika nafasi ya pili na asilimia 21.78 ya kura, juu kidogo kulinganisha na matokeo kiliyoyapata katika uchaguzi wa 2019 ya asilimia 20.77.

**AFP**



Hali ilivyo katika Jimbo la Baden Wurttemberg nchini Ujerumani baada ya kukumbwa na mafuriko ambayo yamesababisha maelfu ya watu kuhamishwa katika makazi yao jana. **PICHA: MTANDAO**

## Zelensky aonyesha wasiwasi dhidi ya Trump

**KYIV,** UKRAINE

GAZETI la The Guardian limechapisha mahojiano ya kipekee iliyofanya na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, ambako anaonya dhidi ya Donald Trump kushinda uchaguzi wa rais wa Marekani na kutupilia mbali uungaji mkono wa kijeshi kwa Ukraine.

Trump aliahidi mwaka jana kwamba ikiwa atamshinda Joe Biden, angekatiza msaada wa kijeshi kwa Ukraine na kumaliza vita ndani ya saa 24.

Wale walio karibu na Trump pia walidokeza mpango anaopendekeza kupeana mikoa ya mashariki ya Ukraine kwa Russia, pamoja na Rasi ya Crimea, kumaliza mapigano.

Lakini Rais Zelensky alisisitiza kuwa nchi yake haitakubali mpango huo, wala haiko chini ya shinikizo la Russia ambayo inajaribu kuilazimisha kuachana na wazo la kujumuika na Ulaya na kujiunga na NATO katika siku zijazo.

Rais wa Ukraine alikiri kwamba kurejea kwa Trump katika Ikulu ya White House kunaweza kuhusisha kukatisha msaada wa kijeshi na kifedha kwa nchi yake, na kwamba Ukraine haiwezi kukabiliana na jeshi la Russia lenye uwezo mkubwa bila silaha.

Alisema jambo hilo haliwezekani kutendeka, lakini likitokea athari zake zitakuwa hatari kwa msimamo wa Marekani katika ngazi ya kimataifa, na kwa sifa ya Trump binafsi, kwani atatajwa kuwa rais aliyeshindwa na ambaye amepunguza makali ya msimamo wa Marekani.

Kuhusu kesi inayomkabili Tramp alisema atakubali kifungo cha nyumbani au jela baada ya jopo la Mahakama ya New York kumkuta na hatia wiki iliyopita katika kesi ya kihistoria, licha ya kwamba itakuwa vigumu wananchi kukubali hilo.

**BBC**

# Claudia ashinda urais kwa kishindo Mexico

**MEXICO CITY,** MEXICO

MGOMBEA wa mrengo wa kushoto uliyo madarakani, Claudia Sheinbaum, ameshinda kwa kura nyingi katika uchaguzi wa urais nchini Mexico ikiwa ni kwa mujibu wa matokeo rasmi ya kwanza yaliyotangazwa na Taasisi ya Taifa ya Uchaguzi (INE).

Claudia atakuwa rais wa kwanza mwanamke kuongoza taifa la Mexico baada ya miongo mingi ya uongozi nchini humo.

Ilielezwa kuwa Claudia alipata kura 58 sawa na asilimia 60, dhidi ya mshindani wake wa upinzani, seneta wa zamani wa mrengo wa kulia Xochitl Galvez, aliyepata asilimia 26 hadi 28 ya kura katika uchaguzi huo, huku mwenyekiti wa INE, Guadalupe Taddei, akibainisha kuwa Jorge Maynez kutoka mrengo wa kati amepata kati ya asilimia tisa hadi 10 ya kura.

Mteule huyo katika taarifa yake ya kwanza ya televisheni baada ya matokeo ya kwanza yaliyotangazwa na INE, aliahidi Wamexico kwamba hatowaangusha.

„Nitakuwa rais wa kwanza mwanamke wa Mexico chama chatu cha 'Movement for National Regeneration' (MORENA) kilishinda kwa wingi wa kura katika Bunge la Congress," alisema.

Baada ya kupiga kura nchini Mexico, Claudia alipongeza siku ya kihistoria, akieleza kuwa hakujipigia kura mwenyewe katika uchaguzi wa urais, lakini kwa mwanzilishi wa mrengo wa kushoto wa Mexico, Ifigenia Martinez, 93, kama kumbukumbu kwa mapambano yake.

Claudia pia alionyesha kufurahishwa na umaarufu wa rais anayemaliza muda wake kwa maoni mazuri kwa asilimia 66. Na kwamba alitegemea kuegemezwa kwa chama tawala cha MORENA, ambacho katika miaka 10 ya kuwepo na washirika wake kilishinda urais, wingi wa wabunge, pamoja na majimbo ishirini kati ya 32.

Katika ujumbe wake baada tu ya vituo vyote vya kupigia kura kufungwa, Xochitl Galvez aliwaonya wafuasi wake dhidi ya ubabe wa wale walio madarakani, akieleza kwamba wanauwezo wa chochote. Ilielezwa kuwa wapigakura milioni 98.3 walisajiliwa kwenye orodha ya wapiga kura. Na kwamba Wamexico pia walipigia kura Bunge la Congress na Seneti, magavana katika majimbo tisa kati ya 32, wabunge wa ndani na nameya.

**RFI**

# TABORA UNITED YAIWINDA JKT TZ KUELEKEA PLAY OFF

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Tabora United kimesema kipo katika mikakati ‚kabambe' kuhakikisha inabaki kwenye Ligi Kuu Bara kwa kupata matokeo mazuri watakapokutana na JKT Tanzania katika mechi za mchujo.

Ofisa Habari wa Tabora United, Christina Mwagala, alisema viongozi wa timu hiyo wanajipanga na kujiimarisha kwa sababu wanataka matokeo chanya katika mechi zote mbili huku wakiwataka mashabiki Tabora kutokuwa na wasiwasi.

Mwagala alisema mashabiki wanatakiwa kufika uwanjani kuishangilia timu yao baada ya kufanya maboresho ili kumaliza mechi hizo kwa furaha.

„Wana-Tabora wameshaona ladha ya Ligi Kuu, kwa hiyo sisi kama viongozi tutapambana kuhakikisha msimu wa 2024/25, mkoa wa Tabora unaendelea kuwa kwenye ramani, kuwapo hapa katika mechi hii ya mchujo ni kama fundisho, na kwa sababu tumepata changamoto, halafu imetupa fursa hii ya kujiuliza ni lazima tuitumie vizuri," alisema Mwagala.

Alikiri mechi haitakuwa rahisi kutokana na ubora wa JKT Tanzania, lakini watakachofanya ni kuimaliza mechi nyumbani kwanza, ili kurahisisha kazi watakapokwenda katika mchezo wa marudiano.

"Tunajua haiwezi kuwa ‚play off' nyepesi, kwa sababu tunakwenda kukutana na JKT Tanzania, ambayo nayo inataka kubaki, na katika mechi hii tutaanzia nyumbani na kumalizika ugenini, hivyo tunataka tumalize biashara hapa hapa Ali Hassan Mwinyi ili kurahisisha kazi ugenini," aliongeza.

Alisema kikosi cha timu hiyo kinaendelea vyema na maandalizi ya mechi hiyo, huku kikiwa na wachezaji wote waliosajiliwa.

Mshindi wa jumla wa mechi ya mchujo kati ya Tabora United dhidi ya JKT Tanzania atakwenda kucheza mechi nyingine ya ‚play off' dhidi ya Biashara United kutoka Ligi ya Championship, ambapo timu itakayoshinda mechi zote mbili, itapanda Ligi Kuu au kubaki, kutegemea na ilipotoka.

## Prisons kuongeza mastraika, viungo

**Na Shufaa Lyimo**

MABOSI wa Tanzania Prisons wamesema wanatarajia kuboresha kikosi chao kwa kusajili washambuliaji na viungo wapya kwa ajili ya msimu ujao, imeelezwa.

Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ajabu Kifukwe, alisema safu hizo zilionyesha mapungufu katika mechi za msimu uliopita wa Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo wamedhamiria kujiimarisha zaidi.

"Tutasajili wachezaji ambao wataziba mapengo katika safu hizo ambazo msimu uliopita zilionekana zina mapungufu, tunataka kurejea katika soka letu la ushindani," Kifukwe alisema.

Kifukwe alisema tayari wameshapokea ripoti ya ufundi kutoka kwa Kocha Mkuu, Hamad Ally, na walipanga kuanza kuifanyia kazi jana.

"Matarajio yangu ni kuanza kambi mapema ili kujiandaa na msimu mpya ambao utaanza baadaye Agosti, mwaka huu, ninaamini utakuwa ni msimu wenye ushindani zaidi, tunataka kumaliza katika nafasi ya juu," kocha wa timu hiyo iliyomaliza kwenye nafasi ya tisa na pointi 34 kibindoni, alisema.

## Mabondia 29 Dar waingia kambini

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA 29 waliofanya vizuri katika mashindano ya wazi wameingia kambini kwa ajili ya kupata timu ya mkoa wa Dar es Salaam ambayo inajiandaa na michuano mbalimbali ya ndani itakayofanyika hivi karibuni.

Mwenyekiti wa Chama cha Ngumi Dar es Salaam (DABA), Akaroly Godfrey, alisema kambi hiyo inaendelea vyema na iko chini ya Kocha Mkuu, Ramadhan Mazola ambaye anashirikiana na John Serenge, Money Money na meneja wa timu hiyo ni Deo Joachim.

Aliwataja mabondia walioitwa kambini ni Hamadi Hashim, Emmanuel Karebi, Haji Kudra kutoka JKT , Feisal Omar, Mtemi Ramadhani (Ngome), John Christian, Hafidh Bamtula (Ngome) ,Baraka Balisho, Hussein Chambo (JKT) ,Yusuf Abdallah (Ngome), Mohammed Hassan, Rajab Lukemo na Nassor Abdul wa Azam.

Wengine ni Alex Steven (Ngome), Juma Mageuzi (Ng'umbi), Mordekai Swai (Ngome), Asubuhi Maira (Magereza), Sikuzani Simon (Ngome), Basil Saulo (Ng'umbi), Ally Mazimbo (Nagereza), Rashid Hamis, Idrisa Kisi (Mashikamano) na Tommy Thomas wa Dago Star.

**Wachezaji wa Yanga Princess ya Dar es Salaam wakifurahi baada ya kumaliza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kuifuata Bunda Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa Ijumaa Mjini Musoma mkoani Mara.** PICHA: MTANDAO



## DAR SWIMMING YAOTA MEDALI

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Dar Swimming inaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kushiriki Mashindano ya Taifa ya kuogelea yatakayofanyika Juni 22 na 23, mwaka huu kwenye Bwawa la Shule ya Kimataifa Tanganyika (IST), Dar es Salaam.

Mashindano hayo yatashirikishi waogeleaji kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Michael Livingstone, alisema maandalizi yanaendelea vyema na anaamini wachezaji wake watafanya vizuri katika mashindano hayo ambayo yanatarajiwa kuwa na ushindani.

**"Tunaendelea kufanya ma zoezi ili kujiweka tayari na mashindano, naamini mwaka huu kutakuwa na upinzani mkubwa kwa sababu yatashirikisha waogeleaji kutoka klabu mbalimbali nchini, tu naomba wapenzi wa mch ezo huu waje kwa wingi siku hiyo kushuhudia bu rudani na vipaji," alisema Living Stone.**

Aliongeza kwa sasa anawapa waogeleaji wake mazoezi ya pumzi ili wapunguze muda katika siku ya mashindano lakini pia anawataka wazazi kuwaruhusu watoto wao kujifunza mchezo huo kama ilivyo michezo mingine.

"Mchezo huu umeendelea kukua na kupata mashabiki tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita, idadi ya Watanzania wanaoshiriki imeongezeka, zamani wazazi na watoto waliogopa kujifunza wakihofia kupoteza maisha yao," Livingstone alisema.

Kocha huyo alisema wanatarajia kufanya vizuri na kutimiza malengo ya klabu kwa kuondoka na medali mbalimbali.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MBAPPE RASMI MADRID
REAL Madrid inapanga kutangaza usajili wa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ufaransa na Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, mwenye umri wa miaka 25, kabla ya michuano ya Euro msimu huu wa joto. **(Fabrizio Romano)**

### BAYERN YAMTAKA FERNANDES
BAYERN Munich imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes, mwenye umri wa miaka 29 akitokea Manchester United. **(O Jogo - in Portuguese)**

### SANCHO AMKATAA TEN HAG
JADON Sancho, mwenye umri wa miaka 24 amesema yuko tayari kurejea katika kikosi cha Manchester United baada ya usajili wake wa mkopo kumalizika Borussia Dortmund lakini kama Kocha, Erik ten Hag, ataondoka. **(Mirror)**

### UNITED NA BRANTHWAITE
KLABU ya Manchester United inamwinda beki wa Everton mwenye umri wa miaka 21, Jarrad Branthwaite, ambaye thamani yake ni kati ya pauni milioni 60 hadi 70. **(Sky Sports)**

### VILLA YAMTAKA GALLAGHER
KLABU ya Aston Villa inavutiwa na kiungo wa kati wa Chelsea, Conor Gallagher, mwenye umri wa miaka 24. **(Independent)**

### ZETTERER ANUKIA CITY
MABINGWA wa Ligi Kuu England, Manchester City, wanafikiria kumnunua mlinda mlango wa Werder Bremen, ambaye ni raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 28, Michael Zetterer. **(Sport Witness)**

### BRADLEY KUULA LIVERPOOL
LIVERPOOL inapanga kumpa mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ireland Kaskazini, Conor Bradley, mwenye umri wa miaka 20, mkataba mpya uliooboreshwa. **(Mail)**

### MASON KUMRITHI FELIX
KLABU ya Manchester United inazingatia mkataba wa kubadilishana unaohusisha mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, mwenye miaka 22 na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno na Atletico Madrid, Joao Felix (24). **(Star)**

### EVERTON, WEST HAM VITANI
EVERTON pamoja na West Ham wameanza mazungumzo na mabosi wa Burnley kuhusu mpango wa kumnunua beki Mfaransa mwenye umri wa miaka 22, Maxime Esteve. **(L'Equipe)**

### NISTELROOY AITAKA LEICESTER
MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United, Ruud van Nistelrooy, mwenye umri wa miaka 47 anagombea nafasi ya kuwa kocha mpya wa Leicester. **(Mirror)**

## DONDO SOKA MAGAZE LAYA




# VINICIUS JR: NATAMANI KUBAKIA MADRID MILELE

●●● Hata hivyo anahofia kukosa 'baraka' za Flamengo ambayo ni...

**MADRID,** HISPANIA

VINICIUS Junior alidai anataka kubaki Real Madrid 'milele' baada ya kufunga bao katika ushindi wa fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Borussia Dortmund.

Miamba hao wa Hispania walinyanyua kombe hilo kwa mara ya 15 hapo Jumamosi usiku, shukrani kwa mabao ya Dani Carvajal na Vinicius.

Ushindi wao uliwanyamazisha maelfu ya mashabiki wa Dortmund waliosafiri ambao walikuwa na matumaini ya kumaliza kusubiri kwa miaka 27 kubeba kombe la pili la Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Mshambuliaji huyo wa Brazil, Vinicius alipachika jina lake kwenye ukurasa wa mabao katika dakika ya 83 na kufunga kwa mara ya pili kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kupachika bao la ushindi dhidi ya Liverpool mwaka, 2022.

Mkataba wa Vinicius na Madrid utaendelea hadi mwaka 2027 baada ya kusaini mkataba wa nyongeza Oktoba, mwaka jana na mafanikio hayo yalimfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kuzungumzia mustakabali wake, huku nyota huyo wa La Liga akisema anatumaini kusalia Madrid milele.

Akizungumza baada ya kutwaa taji hilo, alisema: "Nimefurahi sana kutwaa taji lingine la Ligi ya Mabingwa Ulaya na klabu hii ambayo imenipa mengi, ni jambo la ajabu sana, si kila mtu anaweza kulipitia na kulitwaa mara nyingi. Inaonekana ni rahisi kuja hapa na kushinda.

Tuliteseka sana msimu mzima, pamoja na majeraha yote ambayo tumekuwa nayo. Kila mtu amefanya kazi ngumu sana kufika hapa. Nina furaha sana kuwa hapa kwa muda mrefu. Natumaini rais anaweza kuongeza mkataba wangu kwa sababu ninataka kuwa hapa milele na kuendelea kuweka historia kama Carvajal, Nacho, Luka Modric au Toni Kroos.

Wameshinda Ligi ya Mabingwa mara sita na wametuonyesha njia. Nataka kuwa kama wao. Ningependa kustaafu hapa, ingawa sidhani kama watu wa Flamengo wataniruhusu."



# DEPAY KUONDOKA ATLETICO MADRID

**MADRID,** HISPANIA

STRAIKA wa Timu ya Taifa ya Uholanzi, Memphis Depay, amethibitisha kuondoka Atletico Madrid baada ya kuitumikia klabu hiyo kwa muda wa miezi 17 tu.

Depay alijiunga na Atletico akitokea Barcelona ambako hakucheza kwa mafanikio na gundu hilo liliendelea kumwandama, hali iliyopelekea kuvunjwa kwa mkataba wake.

Katika ukurusa wake wa Instagram, Depay ameandika „Sio rahisi kusema ni jinsi gani ninavyojisikia ninapoandika ujumbe huu kwa sababu nafikiri mambo yalitakiwa kuwa tofauti na hivi yalivyokuwa. Labda tuache hilo, tutalizungumzia baadaye;

Akaongeza kwa kuishukuru timu nzima kwa muda wote aliohudumu klabuni hapo.

Kwa kauli hiyo inaonekana wazi hajaondoka vizuri klabuni hapo lakini timu mbalimbali kutoka England, Ufaransa na Uholanzi zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili straika huyo licha ya uwezekano mkubwa anaweza akarejea nchini kwao katika klabu yake ya zamani ya PSV.

# Adarabioyo mali ya Chelsea

**LONDON,** ENGLAND

MLINZI wa kati wa Fulham, Abdul-Nasir Oluwatosin Oluwadoyinsolami „Tosin" Adarabioyo atafanyiwa vipimo vya afya na Chelsea wiki hii kabla ya kusaini mkataba wa muda mrefu wa kuwatumikia wababe hao wa jiji la London.

Beki huyo anatarajiwa kujiunga na The Blues kwa uhamisho wa bure mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa mwezi huu.




Newcastle United pia walikwinda saini ya Tosin, mwenye miaka 26, lakini alishindwa kuiacha Chelsea, ambao wana uhitaji mkubwa wa beki wa kati baada ya Mbrazil Thiago Silva kuondoka viunga vya Stamford bridge.

Tosin amewahi kufanya kazi chini ya kocha anayetajwa kujiunga na Chelsea, Enzo Maresca, akiwa timu ya wakubwa ya Manchester City (2016-2020) kabla ya wababe hao wa Ligi Kuu England kumtoa kwa mkopo kwenda West Bromwich Albion kisha kupata dili la Fulham ilipofika Julai mwaka, 2020.

# Southgate: Shaw ana nafasi EURO

**LONDON,** ENGLAND

GARETH Southgate amesema anaamini Luke Shaw ana „nafasi nzuri" ya kuwamo katika kikosi cha mwisho cha England kitakachoshiriki michuano ya Euro 2024 licha ya beki huyo hajacheza soka la ushindani tangu Februari, mwaka huu.

Mechi ya mwisho ya Shaw kwa klabu au nchi ilikuwa Februari 18, mwaka huu, alipochechemea akiwa na tatizo la misuli mapema katika kipindi cha pili cha ushindi wa mabao 2-1 wakati Manchester United ilipoikabili Luton Town.

Southgate alikiri katika tangazo la muda la kikosi cha mwezi uliopita mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 "alikuwa kinyume" katika nia yake ya kusafiri kwa ndege hadi Ujerumani, huku bosi huyo akipewa hadi Ijumaa usiku kupunguza mchujo wa awali wa wachezaji 33 hadi 26.

Shaw aliripoti mapema kwa kibarua cha England baada ya kumalizika kwa msimu wa nyumbani huku akipambana kujidhihirisha na Southgate alitoa taarifa ya kutia moyo alipozungumza na wanahabari hapo juzi.

"Anaendelea vizuri sana, lazima niseme," alisema Southgate akiiambia TalkSport.

"Tumefurahishwa na jinsi anavyoendelea. Bado kuna kitu cha kufanya kabla ya kuingia uwanjani katika hali ya mchezo.

"Lakini nimefurahishwa sana na kazi anayofanya na timu yetu ya uchezaji wa mwili na madaktari wetu, kwa hivyo, ndio, yuko na nafasi nzuri."

Shaw amecheza mechi 31 za kimataifa na kufunga bao la kwanza katika mechi ya fainali ya Euro 2020 dhidi ya Italia.

Beki wa kushoto ni tatizo kwa England huku, Kieran Trippier, anayetumika kama beki wa kulia, ndiye anayetarajiwa kuanza kwenye Euro 2024 ikiwa Shaw hayupo.

Akisisitiza iwapo inafaa kucheza kamari kuhusu kujumuishwa kwa Shaw hata kama hayuko sawa kabisa, Southgate alisema: „Hilo ndilo jambo tunalopaswa kulifanyia kazi kwa sababu, bila shaka, kama hayuko tayari kwa mechi mbili za kwanza kuna nafasi kwake.

"Lazima uhakikishe una ulinzi wa kutosha katika hali hiyo pia, kwa hivyo kuna mchezo wa namba tutakaocheza kwa siku chache zijazo.

"Ni wazi, yeye ni beki maalum wa kushoto ambaye ni mchezaji wa kiwango cha juu, kwa hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kuchukua nafasi."



HABARI MICHEZO

# MOROCCO AIFAGILIA STARS, BITEGEKO AITWA KIKOSINI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutoka suluhu dhidi ya wenyeji, Indonesia, Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Morocco, amewamwagia sifa vijana wake, akisema wameitendea haki mechi hiyo ya kirafiki iliyochezwa jijini Jakarta juzi mchana.

Stars imetumia mechi hiyo ya kirafiki kujiandaa kuikabili Zambia (Chipolopolo), katika mchezo wa Kundi E wa kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026.

Morocco aliliambia Nipashe ameanza kuona mwanga katika kikosi chake kuelekea mechi ijayo dhidi ya Chipolopolo.

Kocha huyo alisema timu yake ilitawala vipindi vyote viwili na kutengeneza nafasi nyingi, ingawa hawakuzitumia vyema, lakini inaonyesha ni jinsi gani walivyopambana na kushika mafunzo aliyowapatia.

"Ilikuwa mechi nzuri, tuliwapa nafasi vijana wengi, imekuwa vizuri kwangu mimi kwa sababu sasa nitapata machaguo mengi na kikosi kipana.

Katika mechi hii tumecheza vizuri vipindi vyote viwili, tumetawala mchezo, tumezuia presha za wapinzani wetu, tumetengeneza nafasi nyingi, hilo kwangu ni jambo la msingi sana kuliko mengine," alisema kocha huyo.

Aliongeza atayafanyia kazi haraka mapungufu machache aliyoyaona ili kuhakikisha wanakuwa imara kabla ya kukutana na Zambia ambayo pia ina kikosi imara.

"Tunatakiwa turudi tena katika ubao wa mazoezi, tutaenda kutatua matatizo ambayo yameonekana, mechi hii imetusaidia kuangalia mapungufu kabla ya kuwavaa Zambia, hawa waliopo na tukichanganyika na wale ambao hawakuwapo, tutakuwa imara zaidi kwa kuwakabili wapinzani wetu," Morocco aliongeza.

Wakati huo huo, Morocco amemwongeza, Alphonce Bitegeko wa Azam FC katika kikosi chake.

Mbali na Zambia, timu nyingine zilizoko katika Kundi E ni pamoja na vinara Morocco na Niger.

# Mudathir ataja siri ya ushindi

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Yanga, Mudathir Yahaya, amesema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, aliwataka wachezaji kutumia akili zaidi katika mchezo wao wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC ili kubeba taji hilo, imeelezwa.

Juzi Yanga ilifanikiwa kutetea ubingwa wa mashindano hayo kwa ushindi wa penalti 6-5 baada ya mchezo huo kumalizika kwa suluhu ndani ya dakika 120.

Mudathir alisema Gamondi aliwaambia wapinzani wao pia wamejiandaa vizuri kwa ajili ya fainali hiyo hivyo ni akili ya kila mchezaji ndio itaamua mechi.

Aliongeza Gamondi alifahamu mchezo huo usingekuwa mwepesi hivyo lazima nguvu za ziada za kupambana zihitajike.

"Mbali na maelekezo hayo ya kocha, lakini pia ubora wa kikosi chetu umesaidia kuchukua huu ubingwa, tumekuwa na kikosi bora na kila mchezaji yupo katika kiwango kikubwa,"' alisema kiungo wa Timu ya Taifa (Taifa Stars). Aliongeza kwa wanaenda mapumziko na baadaye watarejea kujiandaa na msimu mpya wa mashindano ambayo pia wanahitaji kufikia malengo.

„Tunamshukuru Mungu msimu huu tumefanikiwa kile tulichokipanga, tumecheza robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika, tumetetea Kombe la Ligi Kuu na hili la FA, tunaenda kujipanga kwa ajili ya msimu ujao wa ligi na mshindano ya kimataifa," alisema Mudathir.



Kiungo wa Yanga, Pacome Zouazoa (kushoto), akiruka kuwania mpira dhidi ya mshambuliaji wa Azam FC, Kipre Jr katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa New Amaan Complex, Zanzibar juzi usiku. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## Gamondi: Mkataba wangu umemalizika

INATOKA UK. 24

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema ni kweli mkataba wa kocha huyo umemalizika na tayari uongozi wa klabu hiyo umeshaanza mazungumzo kwa ajili ya kumpa mkataba mpya. Kamwe alisema kama ilivyo kwa wachezaji, Yanga haitakuwa tayari kuona nyota au mwajiri mwingine wanayemhitaji anaondoka.

"Yanga ni timu kubwa, tumejipanga na tumedhamiria kujiimarisha zaidi katika kila idara, kila kitu kitakwenda vyema, hatutaki kurudi nyuma," Kamwe alisema.

Awali Yanga ilisema malengo yao katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ni kucheza hatua ya makundi, lakini ilivuka na kutinga robo fainali, lakini kwa upande wa Ligi Kuu na Kombe la FA, imefanikiwa kutetea ubingwa. Mabingwa hao wanatarajia pia kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame yatakayofanyika kuanzia Julai 20 hadi Agosti 4, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

## Super Sport Utd yamfuata Onana

INATOKA UK. 24

kukataliwa kwa sababu hata yeye mwenyewe tu kabla ya ofa viongozi walikuwa wamegawanyika, wengine wanataka abaki, atolewe kwa mkopo au aondoke ili nafasi yake asajiliwe mchezaji mwengine, sasa imetokea hii, yaani dili likikamilika atauzwa tu," kilisema chanzo chetu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema katika kipindi hiki cha usajili, wapo wachezaji ambao watauzwa, kutolewa mkopo na watakaoachwa kutokana na sababu mbalimbali.

Ahmed alisema uamuzi huo utafanyika kwa sababu ya kuhitaji kujenga na kuimarisha kikosi kuelekea msimu ujao wa mashindano.

"Pamoja na hayo, ukiona mchezaji ameondoka Simba ujue hatumhitaji, tunachotaka ni kuwaongeza mikataba wachezaji wote walio katika mipango yetu. Kwa hiyo ukiona anayeondoka ujue amepisha nafasi ili wengine wasajiliwe," alisema Ahmed.

Simba ilimsajili Onana akitokea Rayon Sports ya Rwanda, ambapo hata hivyo amekuwa akifanya vyema katika mechi chache tu.

Raia huyo wa Cameroon, amekuwa akionyesha kipaji kikubwa katika kusakata kabumbu, lakini baadhi ya mashabiki wa Simba wameonekana hawaridhishwi na huduma yake, licha ya kufunga mabao mawili, Simba ikiichakaza Wydad Casablanca ya Morocco, mchezo uliopigwa Desemba 23, mwaka jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, timu hiyo ikipata ushindi wa mabao 2-0.


Michezo
Jumanne Juni 4, 2024
Nipashe

## Depay kuondoka Atletico Madrid



UKURASA 22

Baadhi ya wachezaji na viongozi wa Yanga wakiwa na kombe la ubingwa wa mashindano ya FA walipotembelea katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar jana. Yanga ilitwaa taji hilo baada ya kuifunga Azam FC penalti 6-5. PICHA: MPIGAPICHA WETU



# Gamondi : Mkataba wangu umemalizika

### Kocha huyo atamba Yanga ndio timu bora Tanzania, awaachia...

Na Faustine Feliciane ,

ZANZIBAR

SIKU moja baada ya kuipa ubingwa wa Kombe la FA, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema ana kila sababu ya kuwashukuru wachezaji wake kwa uwezo mkubwa walioonyesha katika msimu huu.

Chini ya Gamondi, Yanga imetetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kombe la FA na ilitolewa katika hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Yanga ilimaliza msimu wa 2023/2024 kwa kutwaa Kombe la FA baada ya kuifunga Azam FC kwa penalti 6-5, kufuatia timu hizo kushindwa kufungana katika dakika 120.

Akizungumza na Nipashe jana, Gamondi alisema hakuna ubishi Yanga ndio timu bora kwa sasa hapa nchini na hiyo imetokana na namna ilivyopambana katika kila mechi.

Gamondi alisema anawashukuru wachezaji wa Yanga kwa kucheza katika kiwango bora wakati wote na kuongeza hajui hatima yake ndani ya kikosi hicho kwa sababu mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara umemalizika.

„Mkataba wangu na Yanga umemalizika leo (jana), naenda kufikiria kabla ya kufanya uamuzi mwingine, nimefurahi kwa kile tulichokifanya katika msimu huu,“ alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema wachezaji wake walimpa kila kitu na walikuwa wakifuata maelekezo yote na kupelekea kazi yake kuwa nyepesi uwanjani.

„Nimekuwa na wachezaji wenye ubora sana, hii ni sababu mojawapo ya Yanga kufanya vizuri, siku zote usajili mzuri unakupa matokeo mazuri mwisho wa msimu, kwa kweli najivunia sana kufanya nao kazi,“ alisema kocha huyo ambaye ni raia wa Argentina.

INAENDELEA UK. 23

## Super Sport Utd yamfuata Onana

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Super Sport United inayoshiriki Ligi Kuu Afrika Kusini inatajwa kumwania winga wa Wekundu wa Msimbazi, Willy Onana.

Taarifa za ndani zinasema klabu hiyo ya Afrika Kusini tayari imeanza mawasiliano rasmi na Simba kwa ajili ya kufanya mchakato wa kumsajili mchezaji huyo kuelekea msimu mpya wa mashindano.

Chanzo chetu kilisema Super Sport United imetuma ofa ya Sh. milioni 280 kwa Simba ili kumpata winga huyo ambaye amekuwa na kiwango kizuri licha ya kupata dakika chache za kucheza.

„Kuna ofa kutoka Super Sport, wako tayari kutoa Sh. milioni 280 za Kitanzania ili kumtia mikononi winga huyo, ni suala la kuangalia kama biashara hiyo kwako haina madhara.

Onana alisajiliwa kwa mkataba wa miaka miwili, amebakiwa na msimu mmoja, lakini imekuja hii ofa, haiwezi

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002